# Nipashe

Ijumaa Machi 6, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580172

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wanafunzi 184 wakatisha masomo mkoani Pwani kwa kupata ujauzito

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mbowe anena viongozi upinzani kuitwa Ikulu

**AWEKA** bayana msimamo wa Chadema kuhusu Membe, afunguka sakata la vurugu jimboni... *Endelea ukurasa wa 2*




Balozi wa China nchini, Wang Ke, akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio yaliyofikiwa katika kudhibiti ugonjwa wa corona, ikiwamo majaribio ya chanjo mpya itakayoanza mwanzoni mwa mwezi ujao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# China yatoa mwanga wa chanjo ya corona

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MBUNGE LEMA ACHOMOKA LUPANGO**

HATIMAYE Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), jana alipewa dhamana baada ya kukaa...

**UKURASA WA 5**

**MIFUGO 3,000 YALIWA NA WANYAMA MWAKA MMOJA**

ZAIDI ya mifugo 3,000 ya wafugaji wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika wilaya za Tarime...

**UKURASA WA 8**

**FOLENI KUBWA YA MAGARI ENEO LILILOSOMBWA DARAJA**

SIKU moja baada ya barabara ya Morogoro hadi Dodoma kufunguka kwa gari moja kupita kwenye daraja...


## ASKARI POLISI WAUMIZWA KWA VISU

UKURASA 11




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **YANGA YACHOCHEA USHINDI JUMAPILI** UK. 32 **MAONI, KATUNI UK.6**

HABARI KITAIFA

# China yatoa mwanga wa chanjo ya corona

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya China imesema inatarajia kufanya majaribio ya chanjo ya Corona mwezi ujao, yakihusisha matumizi ya chembe hai za damu kutoka kwa mtu aliyeugua na kupona ugonjwa huo ili kumwokoa aliyepata maambukizo mapya.

Sambamba na hilo, imesema kwa sasa inafanya utafiti wa dawa tatu ambazo ziko katika majaribio ya kusaidia kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo.

Balozi wa China nchini, Wange Ke, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa na mafanikio yaliyofikiwa kudhibiti virusi hivyo.

Alisema majaribio hayo yatafanyika ikiwa ni jitijada mbalimbali ambazo nchi hiyo imekuwa ikizichukua za kutafuta ufumbuzi wa mlipuko wa virusi hivyo ambavyo vinaendelea madhara katika nchi mbalimbali duniani.

"Tangu ugonjwa huu ulivyogundulika, Tume ya Taifa ya Afya ya China imekuwa mara kwa mara ikipitia utafiti mbalimbali wa ugonjwa huo, na utafiti wa saba ulitolewa jana (juzi).

"Siku chache zilizopita, Rais wa China alikagua utafiti wa kisayansi na kusema kuwa sayansi na teknolojia ni muhimu katika kuongeza tiba na kupunguza idadi ya vifo.

"Hivi sasa, wataalamu wa tiba wanapima dawa tatu muhimu za kutibu ugonjwa huo, lakini pia wameongeza matumizi ya chembe hai za damu kutoka kwa wagonjwa waliopona ili kufanya majaribio ya kuwatibia wagonjwa wengine wapya na kwa sasa wanatengeneza chanjo ambayo mojawapo itafanyiwa majaribio mwanzoni mwa Aprili mwaka huu," alibainisha.

Ke alisema kwa sasa nchi hiyo imefanikiwa kudhibiti kwa kiwango kikubwa maambukizo mapya ya ugonjwa huo tofauti na ilivyokuwa awali wakati ugonjwa huo unalipuka.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Ke alisema tangu kuzuka kwa ugonjwa huo China, baadhi ya shughuli za uzalishaji zilisimama kwa muda na kusababisha biashara katika baadhi ya nchi, ikiwamo Tanzania katika Soko la Kariakoo, kuyumba.

Alisema muda si mrefu kutokana na jitihada zinazofanyika za kudhibiti ugonjwa huo, matumaini makubwa ya kurejea kwa biashara kama ilivyokuwa awali na kuwatoa hofu wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitegemea kwa asilimia kubwa bidhaa kutoka China.

"Ni kweli kwamba tatizo hili lilisababisha mtikisiko wa kiuchumi kutokana na kusimama kwa uzalishaji China na kusababisha mtikisiko wa biashara za miji mingi, ikiwamo hapa Kariakoo.

"Tunashukuru kwamba kwa sasa baadhi ya shughuli za uzalishaji ambazo zilikuwa zimesimama China zinafanyiwa utaratibu ili zirejee katika hali yake ya kawaida.

"Tuna imani kwamba baada ya uzalishaji China kurejea katika hali yake ya kawaida, katika Soko kuu la Kariakoo hali itaendelea kuwa nzuri," alisema.

Kuhusu wanafunzi 400 wa Kitanzania wanaosoma katika Mji wa Wuhan, Ke alisema kuwa wako salama na kwamba wamekuwa kwenye uangalizi maalum na wanapatiwa huduma zote muhimu.

Tangu mlipuko wa virusi vya Corona utokee China Desemba mwaka jana, watu walioambukizwa wamefikia 90,870 kutoka nchi 72 huku vifo vikiwa 3,112.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi Miriam Shemndolwa ambaye ni mwenye ulemavu msaada wa Sh. milioni 5, ili pamoja na michango mingine zisaidie ujenzi wa nyumba ya kuishi yeye na bibi yake mlezi, Eonica Hiza (katikati), alipokuwa katika ziara yake huko Mombo wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. **PICHA: OWM**

# Mbowe anena kuitwa Ikulu

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amezungumzia kuitwa Ikulu kwa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa nchini na uamuzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumfuta uanachama aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe.

Jumanne, Mshauri Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, aliitwa Ikulu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mazungumzo na Rais John Magufuli.

Mbali na Maalim Seif, viongozi wengine wa vyama vya upinzani waliokwenda Ikulu na kuteta na Rais siku hiyo ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Profesa Ibrahimu Lipumba, na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Baada ya viongozi hao kutoka Ikulu, kuliibuka mjadala kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kutoonekana Ikulu siku hiyo kwa uongozi wa chama kikuu cha upinzani nchini, Chadema.

Alipoulizwa kuhusu suala hilo jana, Mbowe alisema chama chake licha ya kubeba ajenda ya maridhiano ya kitaifa, hakikupata mwaliko wa Ikulu siku hiyo.

Mbowe pia alisema hafahamu ajenda walizoitiwa viongozi wengine wa vyama vya upinzani ambao siku hiyo walipata fursa ya kuteta na Rais Magufuli.

"Sisi (Chadema) hatujapokea mwaliko wowote wa simu au wa maandishi na hatujui wenzetu wamealikwa kwa utaratibu gani na ajenda ilikuwa ni ipi, labda wao ndiyo waeleze. Sisi tulishaongea hadharani na tulishaandika barua ya kutaka maridhiano ingawa mpaka sasa hatujajibiwa," alisema.

**SAKATA LA MEMBE**

Alipoulizwa kama chama chake kiko tayari kumpokea Membe baada ya kuvuliwa uanachama wa CCM, Mbowe alisema chama hicho sasa kina uzoefu wa kupata faida na hasara ya kuchukua wanachama kutoka chama tawala. Alisema chama kimekuwa kikipokea makada hao wa CCM wasioijua na kuamini katika itikadi ya Chadema, bali kufuata maslahi binafsi, na sasa kimechukua tahadhari na hakina haraka ya kuwapokea.

"Chama chetu kimepata faida na hasara ya kuchukua wanachama kutoka Chama Cha Mapinduzi, 2015-2020 tumepata 'experience' (uzoefu) kubeba wanachama kutoka chama kingine ambao hawaijui itikadi yetu, lakini pengine wanaangalia maslahi ya muda mfupi," alifafanua.

Alisema Chadema sasa iko makini na haina haraka ya kupokea wanachama kutoka vyama vingine, lakini akasisitiza kuwa milango iko wazi na hakuna uadui wala urafiki wa kudumu katika siasa.

**VURUGU JIMBONI**

Vilevile, kiongozi huyo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alitoa ufafanuzi kuhusu vurugu zilizotokea wakati wa mkutano wake na wananchi Jimbo la Hai mkoani Kilimanjaro juzi.

Alisema vurugu hizo ni za kupangwa na kwamba anawafahamu wahusika wa vurugu hizo na nyendo zao.

Mbowe alisema watu hao walipelekwa eneo la mkutano kwa mabasi na walifika eneo dakika chache kabla ya kutimu saa 12 jioni, muda ambao alipaswa kuhitimisha mkutano wake.

Alisema vijana hao walifanya vurugu katika mkutano huo licha ya askari polisi kuwapo na waliwapa majina na namba za magari waliyotumia.

"Wale vijana walikuja mapema kwa kuletwa na mabasi maana ni vyema mkajua kwanza 'back ground' (historia). Hata namba za mabasi yaliyowaleta tunazo na tuliwakabidhi polisi.

"Katika muda wa saa 12 wakati wa harakati za kuaga na kufunga mkutano, wakaanza 'ku-shout' (kupiga kelele) na nakumbuka tuliwaambia polisi kuwa "kuna watu wameandaliwa na mnawajua, wanafanya vurugu na mmesimama nao katikati hapo," alisema. Mbowe aliongeza kuwa baada ya vurugu hizo, aliwaomba wanachama wake kutojibu mapigo ili kuepusha uvunjifu wa amani katika eneo hilo, badala yake kutoa vifaa vyao vilivyotumika katika mkutano huo na kuondoka kwa kuwa muda wa mkutano ulikuwa umekwisha.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Salum Hamduni, alikaririwa na vyombo vya habari juzi, alisema hajapokea taarifa zozote za kutokea kwa vurugu katika mkutano wa Mbunge wa Hai.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 184 wapata ujauzito mkoani Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAFUNZI 184 kati ya 2,091 wa shule za msingi na sekondari mkoani Pwani wamekatisha masomo kutokana na kupata mimba kwa mwaka 2019.

Kati yao waliopata ujauzito, wa shule za msingi ni 40 na 144 wa sekondari huku wanafunzi 1,907 wakishindwa kuendelea na masomo kutokana na utoro.

Kutokana na baa hilo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewaagiza wakaguzi wa shule kufuatilia maendeleo ya elimu mara kwa mara.

Alisema wakaguzi hao wanatakiwa kufuatilia ufundishaji wa walimu, utoro na hali ya chakula cha mchana, akisema kuwa ni vikwazo vinavyochochea utoro.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Abdul Maulid, alitoa takwimu hizo za mimba na utoro mjini Kibaha wakati wa kikao cha wadau wa elimu.

"Utoro ni moja ya vikwazo katika suala la elimu katika mkoa wetu, vingine ni umbali mrefu kutoka nyumbani na ilipo shule na wanafunzi kutopata chakula cha mchana shuleni," alisema.

Maulid pia alibainisha kuwa wanafunzi 2,221 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, hawajaripoti shuleni hadi sasa na hawajulikani waliko.

Maulid alisema wanafunzi hao ni kati ya 25,000 waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza kati ya wanafunzi 30,000 waliohitimu elimu ya msingi mwaka jana.

Baada ya kupewa taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Ndikilo, aliagiza wakaguzi wa elimu kuhakikisha wanatembelea shule na kufuatilia maendeleo ya elimu mara kwa mara.

Ndikilo alisema ikiwa wakaguzi watajenga utaratibu wa kutembelea shule mara kwa mara, matatizo yaliyopo yatapatiwa ufumbuzi na kuondoa utoro shuleni.

"Kila mwaka tuna kikao cha wadau, lakini sijawahi kuona taarifa zilizochukuliwa kwa wanaowapatia mimba wanafunzi, tunataka tuone nini kinafanyika kwa wahusika ili tabia hii ikomeshwe na tuondokane na hili katika mkoa wetu," aliagiza.

Ndikilo alisema kila halmashauri inatakiwa kufanya juhudi za kuwasaka wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni hadi sasa na kufika shuleni kabla ya Machi 30.

Alisema ili kufanya vizuri katika suala la elimu, ni vyema kila halmashauri ikajiwekea mkakati bora na wa msingi wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Alisema wakuu wa wilaya na viongozi wa halmashauri wanatakiwa kukaa na wadau wa elimu kujadili namna ya kuboresha miundombinu ya elimu kama ilivyofanyika katika Wilaya za Kisarawe na Kibaha.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, baadhi ya wakuu wa shule, maofisa elimu na wadau wa elimu.

## Mbunge Lema achomoka lupango

**Na Elisante John,** SINGIDA

HATIMAYE Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), jana alipewa dhamana baada ya kukaa mahabusu ya polisi mkoani Singida kwa siku tatu.

Pamoja na kupatiwa dhamana hiyo, Lema ambaye alikamatwa mjini Arusha na kupelekwa Singida kwa ajili ya kuhojiwa, ametakiwa kuripoti tena Machi 24, mwaka huu.

Jeshi la Polisi lilimshikilia Lema kutokana na kile kilichoelezwa kuwa alitoa taarifa za uchochezi wakati wa mazishi ya kiongozi na kada wa Chadema Wilaya ya Manyoni, Alex Jonas, ambaye mwili wake ulikutwa umetupwa nje huku ukiwa umekatwa katwa sehemu mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mteja wake kudhaminiwa, Wakili wa Kujitegemea Hemed Kulungu, alisema Lema ametakiwa kuripoti tena katika kituo kikuu cha polisi mjini Singida, Machi 24.

Kulungu alisema Lema amedhaminiwa na kada wa Chadema ambaye pia ni Katibu wa chama hicho, Wilaya ya Singida Mjini, Geoffrey Irumba.

Wakili Kulungu alibainisha kuwa kulingana na katiba ya nchi, chombo chenye mamlaka ya kumtia mtu hatiani ni mahakama lakini polisi walimshikilia mteja wake kwa siku zote hizo, hali iliyomlazimu awasilishe maombi Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma kutaka dhamana au mteja wake afikishwe mahakamani, lakini baadaye walijulishwa kwamba dhamana iko wazi.

Kulungu alisema baada ya mteja wake kupata dhamana, walielezwa kwamba polisi wanaendelea na upelelezi juu ya tuhuma za mteja wake na utakapokamilika, atafikishwa mahakamani.

Hata hivyo, Wakili Kulungu, alitumia muda huo kuomba polisi kukamilisha haraka upelelezi wa shauri hilo, ili afikishwe mahakamani. Kwa upande wake, Lema ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, aliwashukuru wanachama wa chama hicho Mkoa wa Singida, walioshiriki kwa namna mbalimbali kuhakikisha anakuwa huru baada ya kupata dhamana.




# Samia akoleza moto ajira SADC

**Na Gwamaka Alipipi**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka mawaziri wa sekta ya kazi na ajira wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupambana na tatizo la ajira kwa vijana kwa kuweka mikakati thabiti.

Vilevile amewataka kuweka uwiano sawa kati ya matumizi ya nguvu kazi na teknolojia ili kuhakikisha vijana wa SADC wanaendelea kunufaika na fursa za ajira zinazozalishwa katika nchi zao.

Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa mawaziri wa sekta ya kazi na ajira na wadau wa utatu wa SADC ambao watakutana kwa siku mbili kujadiliana masuala ya kazi, ajira na uhamaji wa nguvu kazi.

Alisema ukosefu wa ajira kwa vijana umebaki kuwa changamoto ya kidunia na kwamba taarifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu mwenendo wa soko la ajira kwa mwaka 2020, zaidi ya watu milioni 187.7 (sawa na asilimia 5.5) duniani hawana kazi.

Aliongeza kuwa takribani wafanyakazi Sh. bilioni mbili (sawa na asilimia 61.12) wanafanya kazi katika sekta isiyo rasmi na zaidi ya watu milioni 267 (sawa na asilimia 22) wenye umri kati ya miaka 15 na 24 hawako kwenye mafunzo wala katika ajira. "Ni vijana milioni 429 (sawa na asilimia 36) tu ndio walioko kwenye mafunzo na walioko katika ajira ni milioni 509 (sawa na asilimia 42). Hii ni changamoto kubwa ambayo sisi SADC kama sehemu ya dunia, inatuhusu na tunalazimika kuweka mikakati ya kupambana nayo," alisema Samia.

Aliongeza kuwa maendeleo ya nchi yoyote huletwa na nguvu kazi ya vijana na kwamba kwa wastani inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 60 ya nguvu kazi katika SADC ni vijana.

"Kwa mantiki hiyo, hatuna budi kuitumia nguvu kazi hii ipasavyo ikizingatiwa kuwa yapo mahusiano makubwa kati ya nguvu kazi hiyo na ukuaji wa uchumi wa nchi zetu na kuondoa umaskini," alisema.

Samia alisema mtu akipata ajira, hupunguza kiwango cha umaskini kwa njia mbalimbali, hivyo SADC haina budi kuwekeza katika kuwajengea vijana uwezo wa kushiriki vizuri na kwa tija katika ukuzaji wa uchumi wa nchi wanachama.

Kuhusu uhamaji wa nguvu kazi, Samia aliwataka viongozi wa SADC kulitengenezea mikakati mizuri itakayowezesha wananchi wa jumuiya kunufaika.

"Uhamaji wa nguvukazi umekuwa na matokeo chanya na hasi katika nchi za Sadc, matokeo chanya ni pale ambapo nchi zetu zinanufaika na uendelezaji wa ujuzi wa nguvu kazi kutoka nchi za nje au zinazoendelea," alisema Samia.

Aidha, Samia aliwataka wakuu hao kufikia maamuzi yaliyo sahihi na kuona ni kwa namna gani Sadc itawezesha nguvu kazi inayohama katika ukanda wa Kusini mwa Afrika kupata fursa za ajira zenye staha pamoja na kuwezesha uhamishaji wa mafao ya hifadhi ya jamii.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema mawaziri hao watakuwa na majadiliano ya siku mbili kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo mikakati ya kisera kuhusu kazi na ajira.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhi tuzo kwa Ofisa Mkuu Mkaguzi wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori, baada ya benki hiyo kuibuka mwajiri aliyetekeleza kwa kiwango cha juu cha mpango wa Taifa wa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu wa Vyuo vya Elimu ya Juu, wakati wa mkutano wa mawaziri na wadau wa utatu wa sekta ya kazi na ajira kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar, Mouldine Castico. **PICHA: OMR**

## Umeme jua waleta neema

**Na Beatrice Shayo,** KOROGWE

WANANCHI wa Kijiji cha Mpale Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga wamesema umeme jua umewasaidia kupunguza matumizi ya mafuta ya taa kwa siku na kuwawezesha watoto wao kusoma kwa usalama ikiwamo kuacha kutumia vibatari.

Wananchi walieleza hayo jana wakati wakizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), ambao walifanya ziara katika kijiji hicho kwa ajili ya kujifunza mradi wa umeme jua uliopo kijijini hapo.

Mkazi wa kijiji hicho, Hassan Bendera, alisema wamekaa kwa muda mrefu bila kuwa na umeme tangu mwaka 1972 hadi mwaka 2017 walipopatiwa nishati hiyo kutoka kwa wafadhili wa kampuni ya Ensol.

Alisema umeme huo umewanufaisha kupata mwanga na watoto wao kujisomea vizuri ikilinganishwa na awali walipokuwa wanatumia mwanga wa kibatari, ambao haukuwawezesha kujisomea kwa muda mrefu.

"Ninashukuru kupata huu mwanga maana nilikuwa na nunua mafuta ya zaidi ya Sh. 1,000 kwa siku maana nina vyumba vinne inanibidi vibatari niviweke mafuta na watoto wajisomee huyu mfadhili ametusaidia kwa sasa nimeachana na vibatari natumia huu umeme ambao naulipia kama vocha kwa mwezi ambao ni Sh. 11,000," alisema.

Bendera alisema faida nyingi waliyoipata na mwanga huo umewasaidia kuongeza kipato kwani wanafanya biashara hadi saa nne usiku na kipindi cha nyuma ilikuwa mwisho ni saa 12 ya jioni.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mpale, Humphrey Mhina, alisema mwanga huo umewasaidia katika ufaulu wa wanafunzi kuna walimu hujitolea kwa ajili ya kuwafundisha jioni na kutumia nishati hiyo.

"Mazingira ya huku kutokana na hali ya hewa inatulazimu kuwasha taa hata kama ni mchana, hivyo imewasaidia wanafunzi kwa kiasi kikubwa kutokuwa katika giza," alisema.

Mhina alisema kuwapo kwa nishati hiyo jadilifu imewaboreshea mazingira walimu kubaki katika kijiji hicho ikilinganishwa na awali walikuwa wanaondoka.

bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK (TZ) LTD** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA**. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **MIZHIM(T) LIMITED** | **HAMUDU SHAH SALUM** | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja na.1 Kitalu "DD" Hati na.124221 ofisi ya ardhi na.5323291 eneo la Mapinga Kerege yenye ukubwa wa mita za mraba 22,299. | **28/03/2020** |

MASHARTI YA MNADA

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa,au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Equity Bank (Tz)Limited
Head Office,
Ohio street-Golden Jubilee Towers,
P.O. BOX 110183,
DAR ES SALAAM
MOBILE; + 255 768985500
Email: info@equitybank.co.ke

156570

# KUMBUKUMBU



Leo tarehe 06 Machi 2020, umetimiza miaka miwili baba yetu mpendwa **Mzee Guerino Nganyagwa** tangu ututoke duniani

Kama familia tunakukumbuka sana kwa upendo, ucheshi, malezi, faraja, na ukarimu wako katika maisha yetu. Pengo ulilotuachia halitazibika kamwe katika maisha yetu

Unakumbukwa sana na mke wako, watoto wako,wajukuu wako,dada zako,shemeji zako, kaka yako na ndugu na jamaa wote wa ukoo wa Nganyagwa

Ibada ya kumbukumbu itafanyika parokiani Kibada Kigamboni tarehe 06/03/2020 saa kumi na moja jioni

***BABA TULIKUPENDA SANA LAKINI MUNGU KAKUPENDA ZAIDI, ROHO YAKO IPATE REHEMA KWA MUNGU NA IPUMZIKE KWA AMANI.***

115657602

## HABARI KITAIFA

# Mifugo 3,000 yaliwa na wanyama mwaka mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya mifugo 3,000 ya wafugaji wanaopakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti katika wilaya za Tarime, Bunda na Serengeti Mkoa wa Mara, wameliwa na wanyama wakali wakiwamo simba na chui katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Mifugo hiyo iliyokufa kwa kuliwa na wanyama hao ni ng'ombe, mbuzi na kondoo ambayo ndio tegemeo lao la maisha, huku wafugaji hao wakimwomba Rais John Magufuli kuwasaidia.

Wamefikisha kilio hicho kwa nyakati tofauti kwenye mikutano ya hadhara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina iliyofanyika vijiji vya Masanga Wilaya ya Tarime, Nata wilayani Serengeti na Mariwanda wilayani Bunda mkoani Mara.

Alisema kwa muda mrefu wameteseka na hali hiyo bila kupata msaada wowote kutoka serikalini.

Walisema wamebaki maskini kwani baadhi ya familia mifugo yao imekwisha kwa kuliwa na wanyama, hivyo kuomba msaada wa serikali ili kunusuru familia zao. Mmoja wa wafugaji wa Kijiji cha Nata, Samuel Mahewa, aliomba mwaka huu wa uchaguzi kuwapo nafasi za wabunge wanaotokana na wafugaji ili kupaza sauti zao bungeni kunapotokea matatizo ya aina hiyo ambayo hayajapata nafasi ya kufikishwa serikalini.

Ofisa Wanyamapori wa Kikosi cha Doria na Kupambana na Ujangili Hifadhi ya Serengeti Kanda ya Bunda, John Msekale, alisema wamekuwa wakichukua hatua za kuwahamisha baadhi ya simba na kuwapeleka Hifadhi ya Taifa Burigi Chato kama sehemu ya kupunguza tatizo hilo.

Waziri Mpina alikiri mifugo kuliwa na wanyama, na kwamba serikali ina kila sababu ya kuingilia kati ili kunusuru hali hiyo.

Waziri Mpina ameziagiza Kamati za Ulinzi za Usalama za Wilaya za Tarime, Serengeti na Bunda, vikosi vya doria vya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji vinavyopakana na hifadhi hiyo kuimarisha doria katika vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi hiyo.

Pia Waziri Mpina aliagiza wataalamu kutoka Wizara nne za Tamisemi, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Mambo ya Ndani ya Nchi kuweka mkakati wa pamoja wa kumaliza tatizo hilo huku akiwataka wafugaji kujenga mazizi imara ili kujikinga na wanyama wakali.

# Kinara uchunguzi mkonge awa Katibu Mkuu Kilimo

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli amemteua Gerald Kusaya kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo.

Kabla ya uteuzi huo, Kusaya alikuwa Mwenyekiti wa Timu Maalum iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuchunguza masuala mbalimbali katika tasnia ya zao la mkonge mkoani Tanga.

Kusaya anachukua nafasi ya Mathew Mtigumwe, ambaye atapangiwa kazi nyingine katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu jana, alisema kuwa uteuzi wa Kusaya ulianza mara moja jana.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Kusaya na timu yake waliwasilisha kwa Waziri Mkuu ripoti ya uchunguzi wao kuhusu mkonge, wakifichua ubadhirifu mkubwa wa mali za mkonge ikiwa ni pamoja na nyumba na mashamba.

# Wachangamkia ufadhili masomo India

**Na Romana Mallya**

WAHITIMU na wanafunzi kutoka shule mbalimbali wamejitokeza kuomba kusoma India baada ya nchi hiyo kutangaza ufadhili wa kuwasomesha vyuo vikuu kwa kuwalipia ada, malazi na chakula.

Masomo yaliyopo kwenye ufadhili huo ni pamoja na usanifu majengo, sanaa, biashara, uhandisi, sayansi jamii, sheria, utawala na uongozi, famasia na sayansi.

Balozi wa India nchini, Sanjiv Kohli, alisema jana jijini Dar es Salaam wakati vyuo 15 kati ya 40 vya nchini humo vikitoa fursa ya kukutana na wanafunzi wa kitanzania ili kuwapa maelezo namna ya kutuma maombi yao yatakayowawezesha kuingia kwenye ufadhili huo.

Alisema India imekuwa ikitoa fursa hiyo kila mwaka kutokana na ushirikiano uliopo baina yake na Tanzania.

"Tumekuwa tukishirikiana na Tanzania katika nyanja tofauti ikiwamo teknolojia na kujengeana uwezo," alisema balozi huyo.

Alisema wale ambao watapata fursa hiyo, Ubalozi wa India nchini utawawezesha pindi wawapo nchini humo wajione wako nyumbani.

"Hapa kuna vyuo 15 kati ya 40 vya India ambavyo vipo kwenye ufadhili huu. Vimekuja hapa ili wanafunzi wa Kitanzania wapate maelezo ya kina namna ya kuomba kujiunga," alisema.

Balozi huyo alisema kila mwaka wamekuwa wakitoa ufadhili kwa wanafunzi wa Kitanzania kati ya 400 na 550 na Tanzania ni mnufaika mkubwa.

Kiongozi wa msafara kutoka kampuni ya EdCIL ambayo inajishughulisha na masuala ya kuwezesha wanafunzi kusoma nchini India, Nikhil Mahajan, alisema Wizara ya Elimu India imekuwa ikitoa Dola za Marekani 3,500 kila mwaka kwa ajili ya kulipia ada, malazi na chakula kwa wanufaika.

Alisema wahitimu na wanafunzi waliojitokeza jana wamepata fursa ya kupata maelezo mbalimbali ya namna ya kujiunga na vyuo hivyo vilivyo chini ya ufadhili huo na visivyo.

Mahajan alisema wanafunzi ambao wataomba kwenda kusoma India watafanya mitihani mtandaoni Mei 14 na wataratibu suala hilo kwa kushirikiana na ubalozi wa India nchini Tanzania.

Mwanafunzi wa Kidato cha Sita, Alfan Ibrahimu, kutoka Shule ya Sekondari Azania, alisema wanafunzi ambao watafanya vizuri mtihani huo, wameambiwa wataingia kwenye ufadhili.

"Kwa ambao hawatafikia vigezo vya ufadhili walivyoviweka, watatakiwa kulipia asilimia 50 na wao wataweka asilimia 50, hiki ni kitu kizuri ndiyo maana nipo hapa kuhakikisha ninakuwa miongoni mwa wanafunzi watakaosoma India kwa ufadhili," alisema.

Mhitimu wa kidato cha sita mwaka jana, Gladnes Kivamba, alisema amepata fursa ya kuomba kujiunga na vyuo mbalimbali nchini India kwa sababu hakuna malipo yoyote ya uombaji.

"Hii ni fursa nzuri, ninatoa wito kwa vijana wenzangu wafike hapa ili waweze kuwa miongoni mwa watu watakaokwenda kusoma nchini humo, ninapendelea zaidi sekta ya afya hivyo nimeomba mafunzo hayo," alisema.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji mazingira yenye fursa sawa kwa wote

**JUMAPILI** ni siku maalum kwa wanawake duniani, hivyo tunawapongeza kinamama ambao wakati mwingine wanaitwa jeshi kubwa kwa vile ni mashujaa katika kukabiliana na changamoto zilizo kwenye karibu nyanja zote.

Hongereni wanawake mmestahili kupewa siku yenu ndiyo maana Umoja wa Mataifa (UN) uliwasikia kwa vile kwa miaka mingi changamoto zenu hazikushughulikiwa na matatizo ya kinamama na mabinti hayakutatuliwa kwa jitihada zinazostahili.

Na hata sasa tatizo ya ukandamiza na unyanyasaji kijinsia limekuwa kubwa na ndicho chanzo cha kuongezeka njaa, udumavu, umaskini, vifo vya wazazi, wajawazito na watoto wachanga.

Ndiyo maana serikali imetambua kuwa matatizo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yatatatuliwa tu iwapo wanawake watapewa kipaumbele kwa kuutokomeza ukandamizaji na kusimamia usawa wa kijinsia.

Ni vyema kujikumbusha kuwa suala la kuhakikisha usawa wa kijinsia na kutoa haki sawa kwa wote ni lengo la tano la malengo ya maendeleo endelevu ya UN ya mwaka 2015 hadi 2030.

Kwa hiyo ili kufikia malengo hayo serikali imekubali kwa nia moja kuwa Tanzania itafanya juu chini kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye usawa wa kijinsia. Tunaipongeza serikali kwa kung'amua hilo.

Tunakubaliana na serikali kuwa kusema jambo ni sawa na kulitekeleza ni kazi nyingine. Hata hivyo, tunaamini kuwa serikali iliona, ilitafakari na kuamua kufanyia kazi lengo namba tano kwa hiyo tungependa kuishauri mambo kadhaa ambayo yatasaidia kufikia azma hiyo. La kwanza ni kutunga sheria, kuweka miongozo na sera zinazolinda na kudumisha usawa wa kijinsia.

Tukiishauri serikali kuhakikishe kuwa kama kuna masuala ya kulinda na kufanikisha usawa huo ambayo hayahitaji kutumia gharama kubwa yaanze kutekelezwa kwa wakati tena kuanzia sasa. Eneo hili ni kama kuhamasisha wanawake kujifungulia kwenye huduma za afya na kuwakumbusha kwenda kliniki. Hili linaweza kufanywa na viongozi wa vijiji, kamati za afya, asasi za kiraia zikiwamo taasisi za kidini na walimu shuleni.

Serikali ili ifanikishe usawa wa kijinsia izihimize halmashauri za wilaya kutunga sheria ndogo ndogo zinazokataza mila kandamiza zinazowaingiza watoto kwenye masuala ya ngono.

Mila hizo ni kama kukeketa watoto na wanawake, kuwafanyia sherehe za unyago, kuwaoza ututoni, kucheza ngoma zinazodhalilisha watoto na wanawake vijijini na mijini.

Serikali iondoe vikwazo vyote vinavyowakwamisha watu kufikia usawa kwa mfano kama mabinti wanashindwa kusoma kutokana na kukosa taulo za kujisitiri kila mwezi serikali ihakikishe taulo zinapatikana shuleni kwa gharama nafuu.

Ni lazima pia kuwa na wanawake viongozi, hivyo wakati umefika wa kuandaa sheria za kufuatilia uteuzi wa viongozi wa kisiasa kuanzia majina ya wabunge, madiwani na wengine wanaochaguliwa kwenye vyama siasa ili kuwe na ulingano.

Aidha, serikali itunge sheria kuondoa ukandamizaji wa watoto hasa utumikishwa wa watoto majumbani (house girls).

Kuwe na sheria na utaratibu wa taifa kuujua na kuuthamini mchango wa mwanamke katika familia na jamii, hasa kinamama ambao hawana ajira na kuachana na mazoea ya kuwaita magoli kipa na kuwanyima haki zao iwapo ndoa zitavunjika.

Tanzania ni taifa ambalo wanawake ni wengi kuliko wanaume kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2012 idadi ya wanawake ni zaidi ya asilimia 51, hivyo wanahitaji kuwa na huduma bora kwenye uzazi ili mama na watoto wawe salama, lakini kuwapa huduma bora na rafiki za uzazi wa mpango vijana hasa wanawake ili kufikia hatua za usawa wa kijinsia tunazozitazamia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwendokasi huduma ya msimu kiangazi tu ?

**KILA** inaponyesha mvua, iwe ndani ya Dar es Salaam au mikoa jirani, ni lazima utaona tangazo la Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), kuwa eneo la Jangwani halipitiki na huduma za usafiri kwenda katikati ya jiji, Posta na Kariakoo, zimesitishwa.

Hilo linatokana na ukweli kwamba, kituo kikuu cha mabasi hayo kiko eneo la Jangwani, ambako kuna wakati mvua inakuwa kubwa na mafuriko ambayo imeharibu mali nyingi za mradi huo.

Kwa sasa, eneo la Jangwani kuna magari ya kutoa na kuzoa mchanga na udongo unaojaa kwenye mto unaopita pembeni ya ukuta wa jengo la makao makuu ya mradi huo.

Nakumbuka katika miaka ya nyuma kabla ya kujengwa mradi huo, eneo la Jangwani lilikubwa na maaafa yaliyosababisha mamia ya watu kubaki bila makazi na waliondolewa na kupewa viwanja eneo la Mabwepande, ingawa wengine walirudi kwa madai ya kutaka kuendelea kuishi jirani na Kariakoo, wanakotafuta riziki za kila siku.

Baada ya muda, serikali kwa ufadhili maalumu kimataifa, ilianza ujenzi wa mradi huo ambao katika hali isiyokuwa ya kawaida, ujenzi ulifanyika katika eneo hilo.

Ni kawaida na hakuna kinachotokea. Kwamba eneo liko bondeni na linapata mafuriko ya kila mara, mvua inyeshe isinyeshe kutakuwa na mafuriko. Lakini bado ilijengwa karakana ya magari ya Mwendokasi ambayo yaliishia kuharibika vibaya.

Mbaya zaidi, baada ya mradi huo kukamilika na mabasi kuanza kazi, iliyokuwa Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchikavu (Sumatra) wakati huo, ambayo kwa sasa ni Mamlaka ya Usafiri wa nchi kavu (Latra), ilifuta vibali vya usafirishaji daladala za njia hiyo, kwa kuwa suala la usafiri wa umma lilishatatuliwa.

Kimsingi, mradi huo ni mzuri sana na ulivyoanza ulisaidia kupunguza foleni na watu walisafiri kwa haraka zaidi kiasi cha kuvutia wenye magari binafsi wanaofanya kazi maeneo ya Posta na Kariakoo, kuegesha magari yao na kutumia usafiri huo.

Awali, wazo lilikuwa ni kuwafanya watu wasipeleke magari binafsi mjini na badala yake watumia usafiri huo ambao ni rahisi kwao, lakini kidogo kidogo wengi walirudi kutumia magari yao, kutokana na kushuka ubora wa usafiri huo.

Kwa sasa, huduma za usafiri wa mabasi hayo ni kero zaidi kuliko kuwa suluhisho la tatizo la usafiri, Abiria wanajazana kupita kiasi na hakuna utaratibu mzuri kama uliokuwa awali, wakati magari hayo yameanza kazi.

Swali linalosumbua vichwa vya Watanzania wengi ambao kila mara wakiona wingu angani, wanajua barabara katika eneo hilo halipitiki na kama kuna magari ya mwendokasi, yalikuwa upande wa pili basi hayataweza kuendelea na safari.

Ni mradi uliofanyiwa upembuzi yakinifu na michoro ikaandaliwa na wataalamu waliowezesha fedha kutolewa, hata mradi kuanza kazi, lakini cha kushangaza ni kwamba hawakujali mambo mengi ya msingi ya kuhakikisha wanaepuka mafuriko hayo ya Jangwani.

Wananchi wa kawaida kabisa wasio na utaalam wa ujenzi wanatoa suluhisho kuwa yangejengwa madaraja ya juu na karakana ingetafutiwa eneo jingine au ijengwe juu zaidi, lakini haikufanyika hivyo matokeo yake ni sawa na mtu aliyekwenda kujenga nyumba yake kwenye chanzo cha maji. Sasa kama kila mara wananchi waliojenga kwenye vyanzo vya maji wanaondolewa, iweje mradi huo ulijengwe hapo pasipokuzingatia ujenzi wa madaraja makubwa ya kuhimili maji hayo?

Ushuhuda wangu katika baadhi ya nchi mbalimbali, kuna ujenzi kama huo, lakini miundombinu imejengwa juu kiasi ambacho hata mafuriko yawe mengi kiasi gani hakuna uharibifu.

Kwa ujumla, suluhisho la mafuriko hayo kila mwaka ni kujenga upya miundombinu hiyo, lakini kwa sasa ni hasara, kwa kuwa hata gereji yenyewe haiwezi kutumika kutokana uharibifu au usalama wake.

Kama wananchi waliondolewa kunusuru maisha yao na walikuwa wanaishi eneo lisilotakiwa, iweje mradi huo ulikwenda kujengwa kwenye eneo hilo pasipo kuangalia viwango vya ubora kulingana na hali ya eneo husika?

Kutokana na hayo yote, uzuri wote wa mradi umebaki historia na kuwa wa msimu wa kiangazi pekee huku magari mengi yakiwa yameharibika na kama kungekuwa na usafiri wa daladala naamini abiria wengi wasingejali foleni wangepanda magari hayo.

# BARUA & MJADALA

## *Siku ya kinamama kushikamana*

**Mhariri,**

*NI wakati wetu kinamama kufurahi na 'kujiachia' maana ni siku yetu. Robo karne kamili inafika, tangu tukutane kule Beijing China tukikiwa na ajenda nzito sana, kupia kiasi.*

*Hapo binafsi na wenzangu tutakuwa wachoyo wa fadhila, kama hatutomwagia sifa mama yetu mpendwa, Getrude Mongella, aliyeongoza jahazi la kikao kule Beijing, China.*

*Kupitia gurudumu hilo tunalosukuma, tunapaswa kujipanga kikamilifu, walio wadogo kwa umri wanawake kijiti kilikofikia waendelee na safari kwa namna ya kuendeleza walikofikia. Kigezo ni kilekile, sote ni kinamama.*


*Kelele zangu si zaidi zinaanzia kwa mabinti walio shuleni. Huko ndiko kuna majonzi na vilio. Ukianza kwa walimu wao wanakosa usingizi kupitia sababu hiyo na inaenda mbali, kwa wazazi hadi halmashauri mbalimbali.*

*Utasikia simulizi katika mipango yake ya maendeleo, ni nadra usisikie simulizi za ujenzi wa mabweni kwa ajili ya shule za sekondari. Hiyo ndio hali halisi inayotawala.*

*Hapo ndipo ninaporejea katika mtazamo, ni namna gani tutakabili au kumwendeleza mwanamke, inajumuisha kuzikwepa hizo mimba ninazozizungumzia.*

*Mbinu yetu kuu kinamama ni kuwapo ubia kati yetu, bila ya kujali unatoka wapo na huyu ni nani, kigezo kikuu ni uanamke wetu. Tunashikana mkono kuangalia namna gani tunaweza kuinuana kufika mbali. Inawezekana, kinamama tukidhamiria.*

**Subira Binti Hamidu, Kisarawe**




# Kweli kinamama wako 'fiti'

KUSAKA UCHUMI, WATIWE MOYO

**Na Sabato Kasika**

WANAWAKE wameamua kuja na kaulimbiu inayoashiria kuwa wamekuwa na mwamko wa kutosha katika kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kujikomboa kiuchumi.

Kuna kaulimbiu isemayo 'Mwanamke Akipewa Fursa Anaweza.' Sasa wameachana na ile ya 'mwanamke akiwezeshwa anaweza' wakidai kwamba uwezo wanao hawataki kuwezeshwa.

Hivyo ndivyo wanawake kutoka katika kata mbalimbali za wilaya ya Ilala wanavyodai, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo yanafikia kilele chake keshokutwa.

Wakiwa katika maadhimisho hayo yaliyofanyika Jumanne wiki hii, wakishirikisha vituo vya Taarifa na Maarifa, vilivyo chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ukishuhudia, wanasema wanataka fursa za kutosha, ili wainuke kiuchumi na siyo kuwezeshwa.

Kwa kauli hiyo, ni kwamba wasichotaka kusikia ni ile kaulimbiu isemayo 'mwanamke akiwezeshwa anaweza.' Sasa wanataka 'mwanamke akipewa fursa anaweza', kwa vile wameshavuka hatua ya kuwezeshwa.

Hii inaonyesha, ni jinsi gani wamethubutu na kuwa wajasiri katika kuangalia na kuzitumia fursa zilizopo sasa nchini, badala ya kusubiri kuwezeshwa ndipo wafanye kitu.

Kwa kauli hiyo, ni kwamba wanaonekana kujiamini na kujihakikishia kuwa wanaweza kujiletea maendeleo kwa kufanya shughuli mbalimbali, zikiwamo biashara ndogo za kati na kubwa.

Ni dhahiri sasa, kwenye suala la kuwezeshwa, wanawake wamelipa mgongo na wanachotaka ni kupata fursa tu, hawana habari na kuwezeshwa, kama zamani.

Kwa muda mrefu, kundi hilo limekuwa likidai kuachwa nyuma katika harakati za kufanya shughuli mbalimbali, kwa ajili ya kujikomboa, kwa kisa cha kukosa uwezeshaji ambao sasa nuru yake inaanza kuonekana.

Ninaamini sasa, wanawake wanajiamini na kujihakikishia kuwa wanaweza kujiletea maendeleo kwa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwamo biashara ndogo, za kati na kubwa.

Pamoja na hayo, bado wanahitaji kutiwa moyo na kuwaonyesha fursa zaidi zilizopo ili wazichangamkie kwa kutambua kuwa sasa wana uwezo wa kufanya shughuli za maendeleo, bila ya kutegemea upande wa pili.

Wapo baadhi ya wanawake, ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuwahi na kufanyia kazi fursa mbalimbali, zikiwamo za uwekezaji katika biashara. Wote hawa nao watiwe moyo.

Ninasema hivyo, kwa sababu wao ndiyo wanaoumia zaidi, pale uchumi wa familia unapotetereka na hawapendi watoto wao wakose mahitaji ya msingi. Hivyo wanahangaika, kuhakikisha uchumi unakuwa imara.

Kwa hiyo uboreshaji kipato cha familia ni miongoni mwa majukumu ambayo wanawake wanayafanya kwa kutafuta kila mbinu, ikiwamo kujishughulisha kupata kipato cha kuhudumia familia zao.

Pamoja na hayo, jambo la msingi zaidi ni kuwapa elimu ya ujasiriamali, kwani wapo baadhi yao wamekuwa wakianzisha biashara bila kujiandaa kimaarifa na mwisho wa siku zinakufa.

Ninaamini kwamba, wakielimishwa jinsi ya kufanya biashara na kutunza fedha, taarifa za biashara na uandaaji wa uboreshaji wa biashara na utafutaji wa wateja, watakuwa katika mazingira mazuri ya kuimarisha biashara zao.

Hivyo ndivyo wataalamu wa biashara wanavyoshauri kuwa yafanyike hayo, badala ya mtu kuingia mzima mzima katika biashara fulani na kujikuta amepata hasara na kukata tamaa.

Katika mazingira ya aina hiyo, wapo baadhi ya wanawake wanaoanzisha miradi bila ua kipengele cha ubunifu, kwa kuona wenzao wanaifanya na kudhani wanaweza na kuimudu, kumbe matokeo yake wanaishia njiani.

Kwa hiyo wanapotafuta fursa, ni muhimu suala la elimu ya biashara likapewa kipaumbele, ili lilete mabadiliko kwenye shughuli zao wanazofanya au wanazotarajia kuzifanya.

Pamoja na elimu, ni vyema kukawapo ushirikiano wa karibu kutoka kwenye familia kwa ajili ya kuwatia moyo badala ya kuwakatisha tamaa ili hatimaye wanachokifanya kiweze kuzaa matunda.

Watu wa karibu kwenye jambo hili wanaweza kuwa waume zao, na ndiyo wanaotakiwa kuhakikisha biashara za wake zao zinaimarika, na kufanya hivyo ni sawa na kuruhusu fursa hiyo kuwa na manufaa.

Aidha, kuna tatizo lingine la baadhi ya wanawake kuvutiwa na vitu mbalimbali hata kama hawana uwezo kifedha na kulazimika kukopa kwa ajili ya biashara na kumbe lengo ni kununua vitu hivyo.

Hilo analikemea Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Ilala, Francisca Makoyo, kwamba wanawake wanatakiwa kujitambua kifikra na kuchukua hatua za kufanya shughuli za kuwainua kiuchumi.

Ushauri kama huu ni wa muhimu kwa ajili ya maendeleo ya mwanamke kiuchumi, hivyo kinachotakiwa ni suala la kutafuta fursa liambatane pia na kujitambua kifikra ili wajiletee.

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Foleni kubwa ya magari eneo lililosombwa daraja

**Na Idda Mushi,** GAIRO

SIKU moja baada ya barabara ya Morogoro hadi Dodoma kufunguka kwa gari moja kupita kwenye daraja la muda eneo la Kiegeya, maarufu kama Daraja la Mkange, wilayani Gairo, imeibuka changamoto ya foleni kubwa.

Jana usiku magari yalianza kupita kwenye daraja la muda lililojengwa na wataalamu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kukamilisha ujenzi huo na kupunguza changamoto iliyokuwapo. Kukamilika kwa barabara hiyo, kumekuja siku tatu baada ya watumiaji kusota na kumfanya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kutembelea eneo hilo.

Nipashe ilishuhudia foleni ndefu ya zaidi ya kilomita 30 kwa pande zote huku kukiwa na mkorogano kwa magari kutaka kupita mawili mawili ili kuwahi kuvuka eneo la daraja.

Pia ilishuhudia wataalamu wakiendelea na utengenezaji wa njia mbadala kama ambavyo Waziri Mkuu aliagiza juzi.

Baadhi ya watumiaji wa barabara hiyo, walishauri askari wa usalama barabarani kuzuia magari mapya yanayokwenda eneo ili kuruhusu yaliyosota kwa siku kadhaa kumalizika kwanza.

Kuhusu agizo la Waziri Mkuu kuondolewa kwa Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Morogoro, baadhi ya wananchi walisema hastahili kulaumiwa kwa kuwa muundo wa mkoa huo ni kama bwawa linalopokea maji kutoka milimani na ndiyo sababu ya miundombinu mingi kuharibika kirahisi ikiwamo ya reli.

Akizungumza na Nipashe katika eneo hilo, Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Patrick Mfugale, alisema kitaalamu makalavati hudumu kwa miaka 25 zaidi ya hapo ndipo majanga hutokea na kwamba daraja hilo limedumu kwa muda huo toka barabara itengenezwe. Alisema barabara ya Morogoro hadi Dodoma imedumu kwa miaka 40 na kwamba serikali iko katika mpango wa kuitengeneza upya kwa kuwa muda wake wa matumizi umekwisha.

Kwa upande wake, Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Fortunatus Musilimu, aliwashauri madereva kutumia badaraba mbadala kwa sasa kuliko wote kupita njia hiyo.

"Ni vizuri madereva watumia barabara nyingine ili kupunguza msongamano maana hapa magari yanaruhusiwa kwa foleni, watumie nyingine badala ya kutengeneza foleni kubwa.

"Kwa sasa tunadhibiti usalama kuhakikisha magari yenye dharura kama wagonjwa, maiti yanapita badala ya kukaa foleni muda mrefu," alisema Musilimu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Azzan Zungu, akisalimiana na maseneta kutoka Ufaransa waliomtembelea ofisini kwake Mtaa wa Luthuli, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# MOI yafundisha mbinu kisasa upasuaji mifupa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa MOI kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Madaktari Bingwa cha Cosecsa, Chama cha Madaktari wa Mifupa nchini Uingereza (Bofas), imeendesha mafunzo ya siku tatu ya mbinu za kisasa za upasuaji wa mifupa ya unyayo na kifundo cha mguu.

Mafunzo hayo yaliyoanza mapema wiki hii, yalishirikisha madaktari wa mifupa kutoka MOI na mataifa mengine barani Afrika kwa lengo la kuwapa mbinu ya kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya matibabu inayobadilika nchini. Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza katika taarifa iliyotumwa kwa vyombo vya habari, alisema MOI imekuwa ikiwapatia wataalamu wake mafunzo ya muda mrefu na mfupi. "Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya nchini hususani kwenye taasisi yetu ya MOI, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha wataalamu wanapata mbinu za kisasa zaidi ili waweze kuwahudumia wagonjwa vizuri na kupata matokeo bora hivyo tunaendelea kutoa msisitizo kwenye mafunzo kwa wataalamu wetu," alisema Prof. Boniface.

Alisema serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kuwapeleka wataalamu nje ya nchi kupata mafunzo hayo hivyo kuleta wataalamu kutoa mafunzo hayo nchini kumeokoa fedha nyingi na wataalamu wengi wamenufaika.

Naye Mkufunzi na Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka MOI, Samwel Nungu, alisema washiriki wa mafunzo hayo wametoka katika nchi za Sudan, Zambia, Zimbabwe kwa lengo la kuwapa utaalamu wa hali ya juu wa matibabu ya kifundo cha mguu na mifupa ya miguu na wakufunzi wametoka nchini Uingereza.

"Tunaunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha tunaongeza idadi ya wataalamu nchini, hivyo tumekuwa tukiendesha mafunzo haya kwa kuleta wataalamu kutoa mafunzo badala ya kwenda nje ya nchi kwa gharama kubwa kupeleka wataalamu wetu kupata mafunzo haya barani Ulaya au Marekani," alisema Nungu.

Kwa upande wake, mkufunzi kutoka nchini Uingereza, Dk. Rick Brown, alisema mafunzo hayo ya siku tatu yanayosaidia washiriki kutoa huduma na upasuaji wa kifundo cha mguu pamoja na mifupa ya unyayo kwa mbinu za kisasa ambazo zitasaidia kuleta matokeo bora kwa wagonjwa.

## Ofisa madini matatani madai kumba rushwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara, inamshikilia ofisa madini mkazi wa mkoa wa kimadini Simanjiro, Dauda Ntalima, kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. milioni tano kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanzanite One.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Holle Makungu, alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukamatwa kwa ofisa huyo wa madini.

Makungu alisema Takukuru mkoani hapa imebaini kuwa Kampuni ya Tanzanite One inayofanya shughuli zake eneo la Mirerani wilayani Simanjiro kwa sasa imesitishiwa shughuli za uchimbaji.

"Kutokana na majadiliano yanayoendelea kati yake na Serikali ya Tanzania kuhusu mikataba ya uchimbaji, Ntalima ambaye majukumu yake ni pamoja na kushughulikia leseni za biashara ya madini," alisema.

Alisema badala ya kusimamia shughuli zote za uchimbaji wa madini akatumia mwanya huo kuomba rushwa hiyo kutoka kwa Mkurugenzi wa Tanzanite One, akidai hatima ya mikataba ya kampuni hiyo ipo mikononi mwake.

Vile vile, alisema baada ya Mkurugenzi wa Tanzanite One ambaye hakumtaja majina kwa sababu za kiuchunguzi kugoma kutoa rushwa hiyo, Ntalima aliandaa tangazo akipiga marufuku wakurugenzi wote wa Tanzanite One na viongozi waandamizi sita wa kampuni hiyo kuingia na kufanya shughuli yoyote ndani ya ukuta wa machimbo ya Tanzanite Mirerani bila kibali chake.

Mtaalamu huyo wa kupambana na rushwa alisema kosa alilolifanya ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Alisema hakukuwapo mtego walioutumia kumkamata bali walitumia taarifa za kiintelijensia.

Alisema Ntalima anatarajiwa kufikishwa mahakamani uchunguzi utakapokamilika, na amewaomba wananchi kuendelea kufichua vitendo vya rushwa kwa kutoa taarifa ofisi za Takukuru.

# Majaliwa asitisha uchimbaji boxite Lushoto

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imesitisha uchumbaji wa madini ya boxite katika mlima wa Magamba wilayani Lushoto, mkoani Tanga, baada ya wananchi kuulalamikia mradi huo kuwa unasababisha uharibifu wa mazingira.

Hivyo, Waziri Mkuu ameagiza viongozi wa serikali wahakikishe wanaimarisha ulinzi katika eneo hilo mtu yeyote asiendeshe shughuli za uchumbaji wa madini hata Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) nao wasichimbe eneo hilo.

Alitangaza uamuzi huo jana, baada ya kutembelea eneo hilo na kuzungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika uwanja wa Shule ya Msingi Mabughai Kata ya Magamba.

Amesema alipokea taarifa kwamba yapo malalamiko kuhusu shughuli za uchimbaji wa madini zinazoendelea kwenye mgodi huo tangu uongozi wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, pamoja na Mbunge wa Lushoto, Shabn Shekilindi.

"Hatuwezi kuendelea na shughuli za uchumbaji wa madini kwenye eneo hili wakati wananchi wanalalamikia uharibifu wa mazingira, unaosababisha na shughuli hii. Serikali yenu ni sikivu, hivyo nawaomba mwendelee kuiamini na kushirikiana nayo."

Kadhalika, Waziri Mkuu ameagiza watu wote waliopewa leseni za kuchimba madini katika eneo hilo wazirudishe serikalini na amemwelekeza Waziri wa Madini, Doto Biteko, asimamie zoezi hilo.

Kwa upande wake, Mbunge wa Lushoto, alisema wananchi hawataki shughuli za uchimbaji wa madini ya boxite ziendelee kwenye mlima Magamba kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Alisema katika mlima huo ndiko kwenye chanzo cha maji kinachotegemewa na wananchi pia mlima huo umezungukwa na miundombinu mbalimbali ya shughuli za kijamii, hivyo kuendelea kwa uchimbaji wa madini kutasababisha athari kubwa ikiwamo ukosefu wa maji.

Awali, Waziri wa Madini, Doto Biteko, amesema eneo hilo la Magamba lina leseni 22 za uchimbani, lakini kutokana na mvutano wa wenye leseni na wananchi, wizara iliamua kusitisha shughuli za uchimbaji hadi watakapokubaliana.



Sheikh Shaban Albashat kutoka Zanzibar, akichangia mada kwenye mkutano wa viongozi wa dini wa kuhusu njia za kukabiliana na ugonjwa wa ebola na virusi vya corona Tanzania, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tanzania, Ufaransa kushirikiana udhibiti uharibifu wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania imeahidi kushirikiana na Ufaransa katika masuala yanayohusu mazingira.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, alitoa ahadi hiyo jana alipokutana na maseneta kutoka Ufaransa waliomtembelea katika ofisi yake ndogo iliyoko Luthuli jijini Dar es Salaam.

"Tanzania inapenda kushirikiana na Ufaransa kwenye masuala ya mazingira, wala msiwe na hofu wala kigugumizi, kuanzia leo tutaandaa maeneo ya vipaumbele ya kushirikiana ninyi na sisi tufanye kazi kwa pamoja," aliahidi.

Mmoja wa maseneta hao alihoji kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na ukataji wa miti na Zungu akawahakikishia maseneta hao kuwa kwa sasa hakuna tena uharibifu wa mazingira likiwamo suala hilo kutokana na wizara kulisimamia vyema suala hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) alisisitiza kuhusu uwekezaji wa nishati mbadala ili kumkomboa mwananchi wa kawaida aliyeko kijijini na teknolojia ya urejelezaji taka.

Maseneta hao walipongeza ukarimu waliopatiwa wakati wa ziara yao nchini na kuishukuru serikali kwa ukarimu huo na kuahidi kushirikiana nao kwa dhati kabisa katika kutatua matatizo mbalimbali ya mazingira kwa pamoja.

# Ushirikiano kukomesha ukatili wahimizwa

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kushirikiana katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, hasa ukeketaji bila kukata tamaa ili kumaliza tatizo hilo ambalo limekuwa likiwakumba watoto, wasichana na wanawake.

Wito huo ulitolewa juzi na Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Francisca Makoyo, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayofikia kilele chake Jumapili.

Maadhimisho hayo yalifanyika Kipunguni kwa kushirikisha baadhi ya vituo vya taarifa na maarifa vya kutoka kata mbalimbali za Wilaya ya Ilala ambavyo viko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Saidianeni kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na hasa ukeketaji ambao unadaiwa kuwapo kwenye baadhi ya kata ndani ya wilaya ya Ilala ili watoto, wasichana na wanawake waondokane na mateso hayo," alisema.

Makoyo alisema kuna Kamati ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ambazo wanatakiwa kuzitumia katika vita hiyo.

"Zitumieni vizuri ili kusaidia kutokomeza vitendo hivyo kwenye maeneo yenu na pia chagueni viongozi watakaokuwa na jukumu la kufuatilia na kutoa taarifa za vitendo hivyo," alisema Makoyo.

Ofisa Maendeleo huyo alisema kwa kufanya hivyo, mpango wa taifa wa kutokomeza matukio ya kikatili kwa watoto, wasichana na wanawake na unaweza kufikiwa na hivyo kulifanya kundi hilo kuwa salama.

Wakati akisema hayo, Ofisa Progamu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, alidai usiri kwenye baadhi ya jamii bado ni tatizo linalochangia kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo.

"Umefika wakati sasa jamii ijadili kwa uwazi na kuwataja wale wote wanaofanya vitendo hivyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao na pia wekeni ulinzi kwa ajili ya usalama wa watoto wa kike," alisema Temba. Alisema ni muhimu jamii kujua namna ya kutoa taarifa kwa wakati, zinazohusu matukio ya ubakaji, ulawiti, ukeketaji na vipigo bila woga, vinginevyo matukio ya aina hiyo yataendelea kuwapo.

"Pamoja na hayo, wanawake wanatakiwa kuwa katika mazingira salama ili waweze kukua kiuchumi, hivyo ni muhimu ziundwe kamati kwenye mitaa ambazo zitakuwa zinatoa taarifa za ukatili wa kijinsia," alisema.

Alifafanua kuwa taarifa hizo zinatakiwa kutolewa kwenye kamati ya maendeleo ya kata ili kutokomeza ukatili huo na kwamba TGNP iko tayari kuzijengea uwezo kamati hizo.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala (wa tano kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi maandalizi ya maonesho ya kimataifa ya utalii katika Ukanda wa Maziwa Makuu na Jukwaa la Uwekezaji katika sekta hiyo, jijini Mwanza juzi, yatakayofanyika Juni 19 hadi 21, mwaka huu, katika Jiji hilo. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Serikali yajivunia mikutano ya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MIKUTANO minne ya majadiliano kati ya wawakilishi wa serikali, wawekezaji na wafanyabiashara katika mikoa minne ya kanda ya ziwa, imeamsha hamasa ya uwekezaji. Mikoa hiyo ni Mara, Simiyu, Shinyanga na Mwanza, kwa maelezo kwamba serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Changamoto ambazo zilielezwa katika mikutano yote ya mikoa ni riba kubwa zinazotozwa na benki na aina nyingine za taasisi za fedha, kodi na tozo ambapo changamoto za urasimu na ardhi hazizungumzwi kwa nguvu tena.

Mawaziri wakijibu hoja wakati wa majadiliano hasa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, kila alipokuwa akihitimisha majadiliano, alikuwa akiihakikisha sekta binafsi kwamba serikali itaziondoa changamoto zinazoharibu mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya biashara. "Tunakubali kuwapo kwa changamoto hizo. Serikali itazitatua tu," aliuhakikishia mkutano wa mwisho katika Mkoa wa Mwanza na kueleza kuwa serikali imejipanga kuweka mazingira bora na wezeshi kwa biashara na uwekezaji kukua.

Josephine Wambura, aliueleza mkutano wa Shinyanga kero ya kodi na tozo katika tasnia ya hoteli na utalii. Alitoa mfano wa 'kodi ya kitanda' na kueleza kuwa inakuwa kodi ya fedha inapotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na inakuwa tozo fedha inapotozwa na halmashauri kwa kitanda kile kile. "Kodi za aina hii inafaa kuangaliwa upya...kuna kodi ambazo ni kero," alisema. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Ashatu Kijaji, alieleza kwamba serikali imefuta kodi na tozo nyingi mpaka sasa, lakini alisema upande mwingine kuna gharama kubwa mno zinazotozwa katika sekta ya ujenzi na kampuni binafsi.

Alisema serikali imeamua kutumia SUMA JKT kuwapunguzia mzigo wa gharama walipakodi wa Tanzania, na kwamba serikali ikitangaza tenda ya ujenzi, gharama zinazowasilishwa na kampuni binafsi ni kubwa mno, na kwamba kwa kawaida gharama zinazowasilishwa na SUMA JKT ni chini ya nusu ya gharama zilizowasilishwa na kampuni binafsi. Serikali inaamua kutumia SUMA JKT.

Pia alifafanua suala la riba ya mikopo inayotolewa na benki na kusema suala hilo serikali inalifuatilia kwa karibu.

Alieleza huko nyuma serikali kupitia Benki Kuu, alikuwa ikizikopesha benki kwa riba ya asilimia 16. Lakini sasa Benki Kuu inazikopesha benki kwa riba asilimia saba. Kijaji alieleza mkutano kwamba serikali inashangaa kuona benki zinawakopesha wateja wao na kuwatoza riba ya zaidi ya asilimia 16.

# Mwitikio mdogo wa kuuza mazao waishtua h/shauri

**Na Stevie Chindiye,** NAMTUMBO

MWITIKIO mdogo wa wakulima kuuza mazao imesababisha Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma kumwagiza ofisa kilimo kuitisha kikao cha wadau wa kilimo kabla ya kuanza kwa msimu wa ununuzi wa mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani.

Hayo yalijitokeza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani katika halmashauri hiyo, ambapo pamoja na maagizo mengine, madiwani walisisitiza kuwapo kwa kikao cha wadau hao muhimu katika uchumi wa halmashauri yao.

Walisema kikao hicho kitasaidia kupeana uelewa na ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya ununuzi wa mazao kupitia mfumo huo mpya wa stakabadhi ghalani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Daniel Nyambo, alisema madiwani wa halmashauri hiyo kwa umoja wao wamemtaka ofisa kilimo wa halmashauri kuitisha kikao cha wadau wa kilimo wilayani humo kwa ajili ya kupeana uelewa juu ya ununuzi wa mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani.

Nyambo aliendelea kueleza kuwa yapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya watu wasioutakia vyema mfumo huu mzuri wa uuzaji wa mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani, wakipita kwa wananchi na kupandikiza chuki juu ya mfumo huu, hivyo ni vyema kuweka kikao cha pamoja na wadau ili kujengeana uelewa na kuelekezana utaratibu wa kufuata wakati wa kuuza mazao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani. Akitoa ushuhuda wa manufaa ya mfumo huo, mkulima na mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namtumbo, Mohamed Runjes, aliishukuru serikali kwa kuanzisha mfumo huo mpya.

Alisema utaratibu huo kwa msimu wa mwaka 2019/2020, alidai atapata fedha nyingi tofauti na misimu ya miaka. Aidha, Runjes aliiomba serikali kuingiza mazao ya mpunga, mahindi, ulezi na njugu katika mfumo wa ununuzi wa mazao katika mfumo wa stakabadhi ghalani badala ya kuingiza la ufuta na mbaazi pekee.

Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo wakazi wake hujishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali kutokana na wilaya hiyo kuwa na rutuba ya kutosha na hali ya hewa ambayo inaruhusu kilimo cha mazao mbalimbali.

# Shule yapongezwa matokeo kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu,** KISARAWE

SERIKALI wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, imeipongeza Shule ya Sekondari ya wavulana ya Christon mkoani humo kwa kusimamia misingi ya taaluma na kuiletea sifa kufuatia matokeo mazuri ya kidato cha nne 2019/2020.

Akizungumza katika mahafali ya pili ya kidato cha nne ya shule ya hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kisarawe, Mtela Mwampamba, mbali ya

kuupongeza uongozi wa shule na kamati ya wazazi, aliwataka wanafunzi kudumisha nidhamu na kuongeza zaidi juhudi ya kujisomea.

"Ufaulu huu ni mzuri na sisi kama serikali ya wilaya tumefurahishwa sana na matokeo yenu ya kidato cha nne. Tunawapongeza walimu, wanafunzi na wazazi kwa kushirikiana kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwa bidii na kufaulu vizuri katika mitihani ya kitaifa," alisema Mwampamba.

Alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani ya kitaifa kidato cha nne na cha pili, na kuwa mfano mzuri katika

Wilaya ya Kisarawe, hivyo kuzitaka shule nyingine kufuata nyayo.

Kwa mujibu wa DAS, shule hiyo mbali ya kuwa mfano wa kuigwa kitaaluma kiwilaya, pia imekuwa ikishirikiana na serikali katika mambo mbalimbali ikiwamo wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka jana, ambapo iligharamia chakula na kuifanya wilaya hiyo kuwa ya kwanza kimapokezi kwa mkoa wa Pwani.

Aidha, alisema serikali imefanikiwa kuiunganisha wilaya hiyo kwenye umeme wa gridi ya Taifa ambapo mwananchi wanalipa fedha kidogo Sh. 27,000 kuunganishwa huduma hiyo.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, August Minja, alipongeza serikali kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuhakikisha kuwa lengo la kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 inatimia.

"Sisi tumeshaanza kutekeleza azma ya serikali kwa vitendo kwa kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya kujitegemea wawe na elimu ya ziada, ukiachilia mbali ile ya darasani ambayo itatoa mchango chanya kwa serikali pamoja na jamii kiujumla," alisema Minja na kushukuru uongozi wa wilaya kwa ushirikiano.





Mkurugenzi wa Huduma za Kibenki wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Augustino Hotay (kulia), akitoa mafunzo kwa baadhi ya waandishi wa habari kutoka Tanzania Bara na Visiwani, kuhusu utambuzi wa alama za usalama na utunzaji bora wa noti na sarafu, wakati wa semina ya wanahabari wa uchumi na fedha yaliyotolewa na Benki hiyo, Tawi la Arusha. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Polisi wawili washambuliwa, wajeruhiwa kwa visu Babati

**Na Allan Isack,** BABATI

ASKARI polisi wawili katika Mji wa Babati mkoani Manyara, wamejeruhiwa kwa kuchomwa kisu na mkazi wa mtaa wa Nyunguu Kata ya Bagara (jina tunalihifadhi kwa sasa).

Chanzo cha ugomvi huo, imedaiwa kuwa ni wivu wa kimapenzi.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, akizungumza na Nipashe jana, Eliminata Joseph, alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika nyumba ya Mchopa iliyopo Mtaa wa Nyunguu.

Eliminata alisema tukio hilo lilitokea baada ya askari hao kufika kwenye nyumba ya mtuhumiwa, kwa ajili ya kumchukua mwanamke ambaye aliachana na askari polisi mmoja kati yao.

Alisema mwanamke huyo baada ya kuachana na askari polisi, alikwenda kuishi na mtuhumiwa nyumba moja kama mke na mume.

"Siku ya tukio hilo huyo, askari alimchukua mwenzake ili kumfuata mke wake wa zamani, ndipo wakachomwa kisu na kujeruhiwa, hivyo walishindwa kumchukua mwanamke huyo," alisema.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa wa Manyara, Joshua Mwafulambo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na alisema wanaendelea kumtafuta mtuhumiwa wa tukio hilo.

Mwafulambo aliwataja askari waliojeruhiwa ni Godfrey mwenye namba H.5871 na Frederick namba H. 9875.

Alisema askari hao walijeruhiwa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali, na wamepatiwa matibabu katika Hospitali ya Mji wa Babati ya Mrara.

"Askari Godfrey alijeruhiwa kichwani, bega la kulia na mikono yote, na amepatiwa matibabu katika Hospitali ya Mrara... pia ameshasruhusiwa kutoka hospitalini, lakini Fredrick bado amelazwa hospitalini kutokana na kujeruhiwa sehemu za kichwani," alisema.

Aidha, alisema mtuhumiwa huyo alitoka ndani ya nyumba akiwa ameshika kisu na kuanza kuwashambulia askari hao, na kuwa chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi.

"Askari Godfrey alikwenda kumfumania mke wake wa zamani nyumbani kwa mtuhumiwa na ndio sababu ya kutokea kwa tukio hilo," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta mtuhumiwa huyo, ambaye alikimbia baada ya kufanya kitendo hicho.

# Prof. Mbarawa awaahidi Arumeru maji

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali itahakikisha wananchi wa kijiji cha Lengijave katika Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, watapata huduma ya majisafi.

Waziri Mbarawa alisema hayo juzi wakati ziara yake ya kikazi kukagua mradi wa maji wa vijiji vitano.

Mradi huo umefadhiliwa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) na kutekelezwa na Shirika la WaterAid.

Mbarawa alitoa kauli hiyo, baada ya Diwani wa Lengijave, Kalanga Laizer, kuomba mtandao wa maji kuongezwa ili huduma ya maji iwafikie wananchi wote, badala ya kuwafikia wachache kwenye baadhi ya maeneo ya kata hiyo.

Kalanga alisema wananchi wa eneo hilo wana tatizo la huduma ya majisafi na salama, hivyo imesababisha kutumia maji yenye kiwango kikubwa cha madini ya fluoride.

Hata hivyo, Waziri Mbarawa alisema serikali inatambua tatizo hilo, na wapo katika utekelezaji wa miradi ya maji ili kutatua tatizo hilo.

Alisema serikali imejipanga kutekeleza miradi ya maji kwa kuwatumia wataalamu wa ndani "forced account" na itasaidia miradi mikubwa kutekelezwa kwa gharama ndogo na mtandao wa maji utawafikia wananchi wengi.

"Ninajua wananchi wa maeneo haya wanapata maji yenye madini ya Fluoride, lakini nawahakikishie wananchi wote wa maeneo haya mtapata majisafi na salama, kupitia miradi ya wizara itakayotumia forced account, nawashauri mtunze miundombinu ya maji na vyanzo vya maji, kwa kuwa tusipovitunza tutakuwa tunapoteza fedha kutekeleza miradi hii," alisema Mbarawa.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amemwagiza Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaohujumu na kuharibu miundombinu ya maji katika mradi huo.

Lomunyaki Laizer, mkazi wa Lengijave, alisema tatizo la maji kwenye eneo hilo limeathiri uchumi wa familia zao, kwa kuwa wanawake wamekuwa wakitumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli nyingine za uzalishaji.

Mradi wa maji wa vijiji vitano ulisanifiwa kwa kutumia teknolojia bunifu ya malipo ya kabla ya kupata huduma, ili kuiwezesha jamii kupata huduma endelevu ya majisafi na salama kwa kutumia mitambo maalumu ya kuchuja maji.

Mradi huo utahudumia wananchi 23,000, lakini hadi kufikia mwaka 2039 utakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi 50,000.

## Taasisi yataka taarifa za afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI isiyokuwa ya kiserikali inayojihusisha na sekta ya afya katika nchi za Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EANNASO), imesema kuwa taarifa zinazohusu upatikanaji wa huduma za afya hazitolewi kikamilifu.

Taasisi hiyo imeeleza kuwa hatua hiyo husababisha hofu kwa watumiaji wa huduma.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Olive Mumba, alisema hayo jijini Arusha, wakati akizungumza katika kongamano la wadau kutoka Kenya na Tanzania kuhusiana na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wananchi wanaoishi katika mipaka ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Alisema nchi sita za EAC zina idadi ya watu takribani milioni 177, ambao wanahitaji huduma bora za afya, lakini wakati mwingine wamekuwa wakilazimika kwenda maeneo ya mbali kutafuta huduma hizo, wakati huduma zinapatikana maeneo ya karibu.

"Magonjwa hayana mipaka ya nchi na eneo la EAC, lipo kwenye hatari ya kupata magonjwa ya aina mbalimbali yakiwamo ya milipuko...pia tuna watu takribani milioni sita wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), hivyo ni muhimu wananchi kuwa na taarifa za uhakika sehemu ya kupata huduma," alisema Mumba.

Meneja Programu wa Taasisi hiyo, Onesmus Mlewa, alisema wamewakutanisha pamoja wadau wanaoishi katika mpaka wa Kenya na Tanzania upande wa Namanga, ili kuwashirikisha mpango wao wa kutoa maoni namna wangependa kupata taarifa za afya.

"Unakuta kuna mwananchi anayeishi na VVU Kenya anatumia dawa za kufubaza makali ya ugonjwa, lakini anataka kusafiri kuja Tanzania ni muhimu awe na taarifa atakapofika Dodoma au Morogoro akihitaji dawa azipate wapi, kwa kuwa taarifa hizi ni muhimu kwa mtu kuwa nazo?"Alihoji Mlewa. Alisema wananchi wamekuwa wakifuata huduma za afya sehemu za mbali, wakati zinapatikana maeneo ya jirani, na kuwa jambo hilo linasababishwa na kutokuwa na taarifa sahihi.



## Mghwira aipa somo jamii ya wafugaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ameitaka jamii ya wafugaji katika vijiji vya Tindigani, Mtakuja na Sanya Station, Wilaya ya Hai kufikiria kuuza mifugo michache na kujenga makazi bora badala ya kuendelea kuishi kwenye nyumba za tembe na tope.

Mghwira alitaka mabadiliko hayo juzi, alipoongozana na kamati yake ya ulinzi na usalama kwenda kukagua nyumba 43 kwenye vijiji hivyo, zilizobomoka na nyingine kuanguka kabisa kutokana na mvua za masika zilizonyesha juzi kwa saa kadhaa zikiambatana na upepo.

"Haina maana kuwa na mifugo mingi wakati unaishi maisha duni, badilikeni fugeni mifugo michache yenye tija ili mjenge nyumba bora mwondokane na kuishi maisha duni.

Zaidi Mghwira alisisitiza kuwa: "Mkiangalia nyumba nyingi zilizobomoka ni nyumba zilizojengwa kwa matope, hii ni hatari katika nyumba ya Alex Sabore ambaye ana mtoto wa miaka minne aliangukiwa na nyumba na sasa yupo ICU (chumba cha uangalizi maalum) cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC."

Akiwa katika Kata ya Kia, Diwani wa Kata hiyo, Yohana Laizer, alimweleza mkuu huyo wa mkoa kwamba kwa sasa wananchi hao wamejihifadhi kwa majirani zao, wakati wakiendelea kukarabati nyumba zao.

Katika Kijiji cha Sanya Station, watu 34 hadi kufikia sasa hawana makazi kutokana na nyumba zao kubomolewa na mvua.

Wakati katika Kijiji cha Tindigani, nyumba nane zimeharibiwa vibaya na Mtakuja nyumba moja imeanguka, huku pia mvua hiyo ikiacha hasara ya kung'oa miti kuua mifugo.

# Utafiti NEEC wabaini mazito katika ajira

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

UTAFITI uliofanywa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), unaonyesha kuwa asilimia 79.9 ya nguvu kazi iliyopo kwenye ajira hivi sasa, iko chini ya kiwango.

Inaelezwa sababu hiyo, ndiyo inayokwamisha kufikiwa kwa malengo ya utoaji wa ajira za nguvu kazi nchini, wakati ambapo taifa likielekea kufikia malengo ya uchumi wa kati wa viwanda na nchi ya kipato cha kati. Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, alitoa tathmini ya utafiti huo juzi katika Manispaa ya Moshi, wakati wa uzinduzi wa mpango wa miaka mitatu wa utoaji elimu ya ujasiriamali kwa wanafunzi wa shule za sekondari za mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha.

Katika taarifa yake, Katibu Mtendaji huyo alieleza kuwa asilimia 12 ya uwiano wa nguvu kazi ya kiwango cha juu inauhitajika, kwa kuwa iliyopo kwa sasa ni asilimia 3.6 pekee.

Zaidi alieleza: "Kuanzishwa kwa mpango wa kutoa elimu ya ujasiriamali katika shule za sekondari na vyuo hapa nchini kutaleta tija na kuongeza nguvu kazi ya taifa wakati ambapo tunaelekea katika uchumi wa kati wa viwanda.

"Kimsingi, mpango huu unakuja baada ya kuwapo kwa marekebisho ya sera ya elimu ya mwaka 2015. Tunaamini mpango huu utatoa fursa kubwa ya kuongezeka kwa nguvu kazi ya vijana watakaoweza kujiajiri wenyenye na kuajiriwa katika sekta binafsi."

Hata hivyo, baadhi ya walimu na wadau wa maendeleo akiwamo Mratibu wa Mradi wa Pro Bono, Eliet Senkoro na Jonathan Kahatano, ambaye ni mwalimu wa Sekondari ya Fanaka Memorial, walieleza kuwa kuanzishwa kwa mpango huo kutasaidia kuibua vipaji na ujuzi wa vijana katika ngazi za shule na vyuo.

Senkoro alisema mpango huo una nia ya dhati ya kuwainua wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na elimu ya juu kujiajiri wenyewe.




Mmoja wa askari wa Jeshi Usu, akionyesha uwezo wake wa kuzuia pikipiki kwa kutumia kichwa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Viumbehai Duniani iliyoadhimishwa katika Chuo cha Kimataifa cha Uhifadhi wa Wanyamapori cha Mweka, wilayani Moshi, juzi.
**PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Idadi ya faru kutambuliwa kwa kanzi data

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TANZANIA imeanza mchakato wa uanzishaji wa kanzi data ya kitaifa ya kutambua idadi ya faru na mifumo ya uhifadhi ili kuwanusuru wanyama hao kutokana na hatari ya kutoweka duniani.

Mkurugenzi wa Wanyamapori, Dk. Mauris Msuha, alisema hivi sasa wanalenga zaidi katika mikakati ya kitaifa ya kuwekeza kwenye sekta ya utalii wa wanyama hao nchini.

Alikuwa akizungumza jana katika mji wa Moshi, alipokutana na wataalamu wa uhifadhi, utalii na wadau wa maendeleo kutoka katika taasisi zisizo za kiserikali.

"Nimekuja kuzungumza na ninyi ili kuweka na kujadili mikakati ya pamoja ya kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa na faru wengi zaidi ili kukuza sekta ya utalii hapa nchini," alisema Dk. Msuha.

Alisema hivi sasa utalii wa faru ni miongoni mwa utalii adimu sana duniani kutokana na uwapo wa nchi chache zenye faru, huku akiwasihi wa Tanzania kuunga mkono juhudi za kuhifadhi wanyama hao. Tanzania imebarikiwa kuwa na faru ambao wamekuwa na umuhimu mkubwa katika sekta ya utalii, ukiingizia nchi fedha za kigeni. Hata hivyo akizungumza katika mkutano huo, mratibu wa faru nchini, Filbert Ngoti, alisema kwa sasa Tanzania ina faru weusi wengi na kumekuwapo na ufuatiliaji wa taarifa mbalimbali.

Kwa mujibu wa Ngoti, kuanzishwa kwa kanzi data hiyo kutawezesha ukusanyaji wa taarifa kwa usanifu zaidi na kuwekwa kwenye kanzi data moja ya taifa.

Alisisitiza kuwa kanzi data hiyo itasaidia kukabiliana na matatizo ya uhifadhi katika taasisi za uhifadhi, kwa kuwa watakuwa na mfumo utakawasukuma kufikia lengo la kuwa na zaidi ya faru 205 nchini hadi kufikia mwaka 2023. Naye Msimamizi wa Mradi wa Faru kutoka Shirika la Wanyamapori Tanzania (WWF), Kolard Kaanda, alisema kazi kubwa ni kusimamia faru kuendelea kuwapo na kwamba kwa sasa tatizo kubwa linalotishia ustawi wa wanyama hao ni ujangili na biashara za wanyama hao.



Kibiti waapizana kila 'shilingi' yao isipotee

Ukurasa 15

# BUFE

Ijumaa Machi 6, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI



MKATABA TTB & NAS...

## Utalii nchini 'kupaishwa' vivutio viwanja vya ndege kibao duniani

Ukurasa 20




JICHO WILAYA MKURANGA...

## AJIRA YA WATOTO INAVYOTIA SIMANZI STENDI YA MABASI, SHULE YAKAA KANDO

Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

BIASHARA

# Maisha mapya Chama Ushirika Nyanza baada JPM kuiengua shimoni taabani

- Meneja Mkuu aonyesha mwelekeo wao,
- Meneja Shughuli akumbuka zama za JPM

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

***IJUMAA iliyopita, ilikuwapo makala iliyobeba simulizi ya mkongwe mwenye undani wa Chama Kikuu Cha Nyanza, tangu mwaka 1955 hadi ilipofika mwaka 1984, Endelea na simulizi za mwandishi wetu, ilivyo sasa .***

CHAMA Kikuu cha Ushirika Nyanza, ni nyenzo ya msingi wa ushirika kwa wakulima katika mkoa wa Mwanza, ambacho kimebeba umaarufu mkubwa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Kwa miaka kadhaa iliyopita, chama hicho kimeyumba kiuchumi, baada ya madai ya baadhi ya watendaji wake kuuza mali za ushirika huo, kwa ajili ya maslahi yao binafsi, wakilenga kuwa matajiri, lakini badala yake waligeuka kuwa mafisadi na waporaji wa mali hizo.

Ni kutokana na hali hiyo, serikali kupitia agizo la Rais Dk. John Magufuli, ilichukua hatua za kuhakikisha mali zote za ushirika zilizouzwa kwa njia za udanganyifu zimerejeshwa.

Inadaiwa kuwapo watendaji waliouza mali hizo, wakitumia mbinu nyingi za kutaka kuwaaminisha wakulima na wadau, kwamba chama kimefilisika.

Serikali ilichukua uamuzi mgumu wa kuchukua hatua kali za kuhakikisha Ushirika Nyanza unafufuliwa na mali zote zilizouzwa, zimerejeshwa.

**MALI ZILIZOREJESHWA.**

Mali za chama kikuu cha ushirika Nyanza zilizokuwa zimeuzwa na kurejeshwa na serikali, ni pamoja na nyumba tatu za wafanyakazi wake zilizopo eneo la Isamilo jijini hapa, jengo la uchukuzi maarufu kama Kauma lenye karakana na kituo cha mafuta.

Mali zingine ni pamoja na viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula Ashoki; cha kusindika mafuta ya pamba Nywela; mkonge pamoja na ghala la kutunzia mizigo, vilivyoko Igogo jijini hapa.

Kaimu Meneja Mkuu wa Nyanza(NCU), Martha Ndetto,katika mazungumzo yake na Nipashe, anasema hali halisi ya ushirika mwaka huu ni kwamba vimeanzishwa vyama vya msingi vya ushirika vya mazao(Amcos) kwa ajili ya kushirikiana na chama kikuu cha Nyanza, ili kuwasaidia wakulima wa pamba kuwakomboa kiuchumi.

"Hali ya ushirika mwaka huu ni nzuri, isipokuwa kuna changamoto zake, mfano vyama vya msingi vya ushirika vya mazao (Amcos)viko 249 katika Mkoa wa Mwanza.

"Lakini, Amcos 228 tu ndizo zimefanya kazi msimu uliopita 2019/2020 katika ukusanyaji wa zao la pamba kwa wakulima na Amcos 21 hazikufanya kazi zilizopo katika Wilaya za Ilemela na Nyamagana jijini hapa pamoja na Amcos za Ukerewe.




Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndyege, akitoa salamu zake kwenye mkutano wa Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza, hivi karibuni.

"Kukosa mashamba ya kulima ndiyo sababu ya Amcos kushindwa kufanya kazi, hivyo zitafanya shughuli zingine, lakini katika Wilaya ya Ukerewe watu wamekuwa wengi.

"Kwa hiyo, tuna mpango wa kuanza kuhamasisha wakulima kuanzia aprili mwaka huu walime zao la kimkakati la Kahawa kulingana na hali ya hewa na ufinyu wa ardhi, mbadala ya kuendelea kulima zao la pamba," anasema Ndetto.

Anafafanua kwamba, pamba katika msimu uliopita 2018/2019 ilizalishwa kwa wingi na wakulima wa Mwanza, lakini msimu huu imepungua kutokana na mvua kuwa nyingi, hivyo zao hilo haliwezi kustawi zaidi.

Anasema katika mwaka 2018/2019 msimu huo, chama hicho cha ushirika kilikusanya pamba kilo milioni 33,ingawa makadirio yake yalikuwa kukusanya kilo milioni 60 na katika msimu wa 2019/2020, makisio yao kwa wakulima yalikuwa ni kulima hekta 82,000 za pamba, lakini kutokana na mvua nyingi eneo lililolimwa pamba ni hekta 47,000 sawa na asilimia 57

Ndetto anafafanua kuwa, idadi ya wakulima wa pamba pekee katika Mkoa wa Mwanza ni 75,000 na kwa sasa wilaya zinazolima zao hilo ni Magu,Misungwi,Sengerema,Kwimba na Buchosa.

**BEI SOKONI**

Ndetto anasema kwamba, katika msimu uliopita bei ya kuuzia pamba ilileta shida katika soko,Serikali ilitoa bei elekezi kwa wakulima na kampuni ya kununua pamba kuwa kilo moja itauzwa sh,1,200,lakini bahati mbaya ghafla bei ya soko la dunia ikashuka na hivyo wanunuzi wakashindwa kumudu bei elekezi na kujikuta wakulima wengi wakikosa wanunuzi.

"Wakulima wengi waliumia baada ya bei ya pamba kushuka kwenye soko la dunia, kwa hiyo hata wanunuzi wa kampuni walishindwa kununua kwa bei elekezi ya Serikali, huwezi kufanya biashara yenye hasara,sababu unataka faida," anasema.

**NYANZA YA 2020**

Meneja Mkuu huyo, anasema Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza 2020, kupitia vyama vya msingi vya ushirika vya mazao(Amcos) kuanzia mwezi huu, tutaanza kukusanya mazao mchanganyiko ya choroko na dengu, katika mfumo mpya wa stakabaadhi mazao ghalani na kuuza kwa njia ya mnada kwenye kampuni binafsi yatakayokuwa yakinunua mazao hayo.

"Lengo letu na serikali ni kuboresha bei ya wakulima wasiendelee kupunjwa, ili waweze kupata faida,kazi ya Amcos ni kukusanya mazao hayo na kuyaweka kwenye ghala kubwa na sisi tutasimamia kuuza kwa njia ya mnada kwenye kampuni binafsi zitakayokuja kununua,kampuni zikishindanishwa litakalotoa bei kubwa ndilo litauziwa mazao," anafafanua Meneja Mkuu.

Anasema, mfumo huo utawasaidia wakulima kunufaika kiuchumi na mazao hayo na kuepuka udanganyifu wa bei, kwani wakulima wakiuza kwa kutumia 'visado' badala ya kupima kwenye kilo ili wapate faida.

**UFUFUAJI VIWANDA**

Ndetto anasema, Nyanza inatarajia kufufua viwanda vyake viwili kwa ajili ya kuchambua

INAENDELEA UK. 15

# Maisha mapya ya Chama Ushirika Nyanza baada JPM kuiengua shimoni taabani

INATOKA UK. 14

pamba na kuzalisha mafuta ya kula vya Manawa na Buyagu mwaka huu na kwamba kiwanda cha Manawa kitachambua pamba na kuzalisha mafuta ya kula na Buyagu kitafanya kazi ya kuchambua pamba.

Anasema kuwa, viwanda vingine sita vitafufuliwa baadaye kwa hatua, vikiwamo vilivyokuwa vikichambua pamba na kuzalisha mafuta ya pamba, ambavyo ni viwanda vya Magu,Buchosa,Nyamililo,kiwanda cha Bukumbi,Nyambiti,pamoja na Ukerewe.

**MENEJA SHUGHULI**

John Masalu, ni Meneja Shughuli na Usafirishaji wa Nyanza, ana ufafanuzi: "Nilianza kazi Nyanza mwaka 1988 kama mhasibu msaidizi hadi sasa nimetimiza miaka 32 ya utendaji kazi wangu.Katika maisha yangu yote sijawahi kufanya kazi nje ya ushirika huu, baadaye mwaka 1994 niliacha uhasibu nikawa Ofisa Shughuli hadi 1999."

Masalu anasema, baadaye mwaka 2000 hadi 2005 akawa meneja wa kanda,ndivyo hivyo mwaka 2006 hadi sasa 2020 akashika nyadhifa ya meneja shughuli na usafirishaji wa ushirika mkoani Mwanza.

Ni simuilizi anazoendelea nazo, huku akiwa na kubukumbu kumpata mfanyakazi mwenzao aitwaye John Magufuli, akiwa Mkemia Mkuu wa Ushirika Nyanza, hadi mwaka 1995, alipoondoka kwenda kugombea ubunge katika jimbo la Biharamulo Mashariki, kisha muda mfupi baadaye, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

Anaeleza uzoefu wake katika ushirika huo ni walikutana na changamoto nyingi, baada ya ushirika kuyumba, hadi hivi karibuni serikali ilipokuja kuinua tena, ikiwamo kurejesha mali zilizotoweka kiutanishi.

"Ila kwa sasa ubora wa zao la pamba umerejea baada ya ushirika kuimarika na sasa utaweza kuajiri wafanyakazi wengi kama zamani. Nyanza ilikuwa na wafanyakazi 5000 lakini hivi sasa wapo 90 tu.

"Lakini jambo ambalo sitalisahau maisha yangu na lilikuwa likiniumiza zaidi ni pale watendaji wakuu wa Nyanza walipouza mali za ushirika,wakasababisha kuyumba,Nyanza haikufirisika isipokuwa mali zake ziliuzwa na watu wachache kutokana na tama za mali,anasema.

**SOKO HURIA**

Anasema kuwa soko huria lilipoingia miaka ya 1998 lilisababisha ubora wa pamba kushuka bei katika soko la dunia na uzalishaji wake, pamba iliuzwa na wakulima bila ya kuchambuliwa kwa kufuata madaraja ya kutengenishwa safi na chafu na kupelekwa kuuzwa.

Hali hiyo ilisababisha pia kukosekana mbegu bora na kushuka kwa uzalishaji wa wakulima badala ya kuzalisha kilo 500 hadi 1000 katika ekari moja ya pamba,wakawa wanazalisha hadi kilo 100 kutokana na soko huria kutofuata kanuni na taratibu za ubora wa pamba wakati wa kununua.

Masalui anasema, madaraja ya pamba hayakufuatwa, kulikuwa na daraja A lenye pamba safi na daraja lenye pamba chafu iliyochambuliwa.

Anasema kwamba kanuni za kilimo bora cha pamba kikifuatwa na wakulima wataweza kuzalisha mazao mengi ambazo anazitaja kuwa ni pamoja na kulima kwa wakati, kupanda kwa mistari,kuweka mbolea shambani na kunyunyizia dawa ya wadudu waharibifu wa zao hilo.

• ***Mwandishi anapatikana kwa anwani ya barua pepe: anthonygervas@yahoo,com,simu +225(0682 86 92 44,kanda ya ziwa.***



Wanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza, kwenye mkutano Mkuu wa chama hicho. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (chini ya mwamvuli), akizungumza na kinamama waliopeleka watoto wao kupata chanjo katika Kituo cha Afya, kilichopo Kijiji cha Muyuyu, ziarani Wilaya ya Kibiti. **PICHA: MTANDAO.**

# Kibiti waapizana kila 'shilingi' yao isipotee

**Na Yasmine Protace, Kibiti**

USIMAMIZI mzuri wa vyanzo vya mapato, mara nyingi umekuwa ukileta maendeleo yanayohakikisha sehemu inakuwa kimaendeleo. Hivyo, kusimamia vyanzo vya mapato ni jambo muhimu.

Katika serikali za mitaa, imekuwa ikihimizwa na viongozi wa juu kwamba kila halmashauri inapaswa kuhakikisha inasimamia vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya kuiletea maendeleo.

Kupitia vikao na mikutano yake, viongozi wakuu ambao ni wakurugenzi na wakuu wa wilaya wamekuwa wakisisitiza miradi yote ya maendeleo inapaswa kusimamiwa vizuri, ikamilike kwa wakati na itumike kuleta maisha chanya kwa wananchi wake.

Dhana hiyo, inaenda sambamba na hitaji la kusimamia kwa makini vyanzo vya mapato walivyonavyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kibiti, Khatibu Chaurembo, anasema wamejipanga kusimamia miradi ya maendeleo, ikiwamo vyanzo vya mapato katika ngazi ya vijiji vyake.

Katika Kikao cha Robo ya Kwanza cha Baraza la Madiwani, Chaurembo, anasema maofisa watendaji wa kata wa halmadhauri hiyo, wanatakiwa kuamka kusimamia miradi yao ya maendeleo, ikiwamo ambayo ni vyanzo vya mapato.

"Ili mapato ya vijiji na halmashauri yaongezeke na kuleta faida kwa wananchi, inatakiwa (maofisa) watendaji kutolala usingizi," anasema.

Chaurembo anasema, Halmashauri Kibiti haiwezi kujiendesha, kama haina vyanzo vya mapato, pia lazima visimamiwe ili vilete maendeleo kwa wakazi wa maeneo hayo.

Anasema, ubunifu unatakiwa kusimamia vyanzo hivyo, ambao kimsingi unafungua milango ya maendeleo yao, ikizingatiwa hata serikali za vijiji zinaendeshwa kwa kutumia mapato hayo yanayohimizwa kukusanywa.

Diwani wa Kata ya Maparoni, Ngachoka Haji, anasema ambako ni ng'ambo ya bahari, anaomba boti iliyokuwapo Maparoni, iendelee kutoa huduma, kutokana na sasa wajawazito na wagonjwa wanatumia usafiri wa mitumbwi kwenda kufuata huduma za kiafya, wakivuka maji.

"Kutokuwapo boti kunasababisha wanakijiji kupata shida na kutumia mitumbwi kwenda kutafuta huduma za afya," anasema Haji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kibiti, Mohammed Mavulla, anasema hadi sasa wamejipanga kusimamia miradi ya maendeleo, sambamba na vyanzo vyake vya mapato.

Anasema, hadi miradi yote iliyoibuliwa inasimamiwa kikamilifu, huku akitoa rai kwa madiwani kusaidia kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao na isiyokamilika, wana wajibu wa kufuatilia ikamilike kwa wakati.

"Uchaguzi unafanyika mwezi huu Oktoba, sasa madiwani mjitahidi kusimamia miradi ya maendeleo, maana katika kampeni mnaweza kuulizwa maswali na mkakosa majibu," anasema.

Mavulla anasema, katika Halmashauri ya Kibiti, kuna miradi zaidi ya 10 inayoendelelezwa katika maeneo mbalimbali.

Kuhusu boti, anafafanua kwamba serikali imewapatia zaidi ya Sh. milioni 100 ya kununua boti, ambayo hadi sasa inafanyiwa kazi.

Anasema, makubaliano ya serikali na halmashauri ni kwamba, boti hiyo inapaswa kutumika katika maeneo ya ukanda wa bahari wa 'delta' kwa ajili ya kufanya doria ili kulinda vyanzo vya mapato, hivyo ni vugumu kuvunja mkataba kwa kujielekeza na mambo mengine.

BIASHARA

JICHO WILAYA MKURANGA...

# Ajira ya watoto inavyotia simanzi stendi ya mabasi, shule yakaa kando

- Wafanyabiashara wawalipa hadi 250/-
- Mahudhurio darasani 'bahati nasibu'
- Uamuzi gani serikalini?...kitendawili

**Na Elizabeth Zaya, MKURANGA**

MWENENDO wa maisha ya watoto wa Kimanzinchana, si dira ya masomoni hata kidogo. Ni mwelekeo wa kuajiriwa, tena katika sura ya vibarua, hasa ndio mbadala wao wa masomo.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika eneo hilo, umebaini watoto kuanzia umri miaka saba hadi 10, wamejikita katika shughuli ndogo za kibiashara katika eneo hilo.

Ni vibarua vya wafanyabiashara wenye maduka makubwa ya bidhaa Kimanzichana na wanapofanikiwa kuuza, hupatiwa ujira mdogo.

Hapo ni uuzaji maji yaliyofungashwa kwenye mifuko midogo maarufu 'Maji ya Kandoro', karanga, soda, maji yaliyofungashwa kwenye chupa na juisi.

Baadhi waloshuhudiwa na Nipashe, wakifanya biashara hizo kuanzia asubuhi mpaka saa 12 jioni na wapo wanaozidi muda huo, ingawa baada ya saa moja jioni idadi yao inapungua.

Baadhi yao, walipozungumza na gazeti, walisema wamekuwa wakifanya shughuli hizo kutokana na ugumu wa maisha katika familia zao, wengi wanaishi na bibi na babu zao, wasio na nguvu ya kutafuta fedha ya kujikimu kwa mahitaji ya kila siku, ikiwamo chakula, mavazi na mengine ya shuleni.

Pia, iligundulika asilimia kubwa hata walipo masomoni, mahudhurio yao ni duni hata Nipashe ilipowadodosa kupata ukweli, walikiri kwamba wanalazimika kuna wakati watoroke au kutumia saa chache baada ya kurudi shule kufanya biashara hiyo.

Ni vipi wanaipata biashara hiyo? Ufafanuzi unakuja kwamba wamekuwa wakizichukua katika maduka makubwa ya wafanyabiashara wa eneo hilo na baada ya kuuza, wanapatiwa ujira kidogo.

Mfano mmojawapo wanaoutoa ni kwamba, soda 10 anazouza, wanapata kamisheni ya Sh.500 na endapo wakibahatika kuuza na endapo wanauza nusu, wanapatiwa Sh.250. Ni kipato kinachofanana kila kitu kwa uuzaji maji.

Mtoto mmoja anasema, endapo anashindwa kuuza kiwango hicho cha soda au maji 10 au nusu yake, huwa hawapatiwi chochote.

"Baba yangu sijawahi kumuona. Mimi naishi na mama yangu tu, yeye anafanya kibarua mashineni na kuna siku nyingine anapata hela na siku nyingine anakosa. Kama akikosa, huwa anatupikia uji tu,"anasema mmoja wao, anayekadiriwa umri wake kati ya miaka tisa na 10,

"Mimi nikirudi shuleni nikikuta nyumbani hakuna chakula, huwa naenda dukani naomba maji ya kuuza na nikipata hela, tunanunulia dagaa au mboga ya majani tunakula na ugali, Kama mama na yeye amepata naiweka ili inisaidie kununulia mihogo ya kula shuleni.





Mandhari ya kijiji cha Mkuranga, ambako watoto wanaharibika. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Bibi huwa anasema nije nifanye na nikipata hela nipeleke nyumbani. Mimi nauza maji yamefungwa kwenye viroba ambayo nachukua dukani na huwa napewa 300 au 400,"anaeleza yake.**

**CHANGAMOTO ZAO**

Mtoto huyo anasema, mbali na kuuza na anapofanikiwa anapata ujira na asipouza anakosa na amekuwa akikutana na za kudhulumiwa na wafanyabiashara hao, ambako anachukua bidhaa za kuuza.

"Wakati mwingine ukipewa soda au maji 10 na ukafanikiwa kuuza yote, unapokwenda kumpelekea hesabu, huwa wanatugeuka, Unakuta anakuambia, sikupi hela kwa sababu uliniibia soda au maji ukazidisha katika hesabu yako," anasema.

"Ukimuuliza niliiba saa ngapi? Anakazana kusema, uliiba kwa hiyo sikupi hela leo. Hiyo uliyoiba imekulipa, kwa hiyo unaondoka hivyo hivyo bila ya malipo hata kama umebahatika kuuza zote,:" anasimulia katika ufafanuzi:.

"Kesho yake tena unarudi, kwa sababu ukikaa nyumbani unakosa chakula kama mama na yeye hajapata." Mtoto mwingine anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka saba, anaeleza yake kwamba anaishi na bibi yake na amekuwa akifanya biashara hizo ndogo na kupata kipato cha kusaidia kujikimu mahitaji ya nyumbani.

"Bibi huwa anasema nije nifanye na nikipata hela nipeleke nyumbani. Mimi nauza maji yamefungwa kwenye viroba ambayo nachukua dukani na huwa napewa 300 au 400,"anaeleza yake.

Nipashe ilipohoji baadhi ya wananchi wa eneo hilo, walikiri kuwapo utumikishaji huo wa watoto kutumiwa na wafanyabiashara.



**SERIKALI MTAA**

Mjumbe wa serikali ya Mtaa wa Lisimalike, Sihota Mchonjo, anasema watoto wengi wanaofanya biashara hizo ni wale ambao ama wanaishi na mzazi mmoja, bibi, babu au wazazi wao waliotengana kabisa.

Pia, anakiri baadhi ya watoto wanaofanya biashara hizo ni wanafunzi na wanawafahamu, huku akiongeza: "Hao watoto tulishawakataza sana wasifanye hizo biashara kwa kuwa pia ni hatari sana kwao.

"Kwa sababu wakati mwingine huwa wananusurika hata kugongwa na magari. Wakiona linakuja wanakimbizana nalo kutaka kuuza," anaeleza Mchonjo, anayefafanua:

" Wakati mwingine unakuta wananing`inia kabisa kwenye gari, yaani ukiona hivyo alivyo mdogo mpaka unasikia tumbo linakukata.

"Ukijaribu kumkataza, hakuelewi na tabia ya watu wa huku akikusikia unamkemea mtoto wake, hiyo ni kesi kubwa. Kwa hiyo, wakati mwingine inabidi umwangalie tu."

**MFANYABIASHARA**

Muuza duka katika eneo hilo la Kimanzichana, aliyejitambulisha kwa jina la Mohamed Ally, anasema wamekuwa wakifanya biashara na watu mbalimbali kadri wanavyoomba na kuelezea shida zao.

"Unasema kwamba tunafanya biashara na watoto. Sisi hatufanyi kazi na watoto tu, tunafanya na watu wote kulingana na mahitaji yao.

"Mtu hawezi kuja hapa akakuomba kibarua akisema hana hata senti ya kula, halafu ukamkataza. Tunagawana hicho kidogo kinachopatikana.

"Maisha ni magumu ndugu mwandishi. Sisi lengo letu ni kusaidiana, angalau akipata hata kidogo kinamsaidia, kwa mfano kwa watoto ambao wanakuja hapa kuomba ni wale ambao wengine unakuta hasomi na wachache ambao akirudi shuleni ndiyo unamuona anakuja," anaeleza

Kuhusu malalamiko ya watoto kutapeliwa, mfanyabiashara huyo analipinga, kwa kutumia kauli: "Kwangu mimi hilo la kuwatapeli watoto ni jipya, sijawahi kusikia. Lakini, siwezi kukataa moja kwa moja kwa sababu tuko wafanyabiashara wengi hapa, labda wanatapeliwa kwa watu wengine."

**DIWANI ALING'AKA**

Diwani wa Kata Kimanzichana, Ally Ndipitipi, anasema anakoishi ni barabarani na kwamba amekuwa akishuhudia namna watoto hao wanavyokimbiza gari kwa ajili ya kuuza bidhaa zao za uchuuzi.

"Mimi kwa sasa, afya yangu siyo nzuri na kama unavyoona nyumba yangu iko barabarani kabisa. Huwa nikikaa hapa nje kupata upepo, nashuhudia kila kitu na nililazimika kumwita Ofisa Mtendaji wa Kata pamoja na wa Kijiji nikawaeleza.

"Wanasema wanalifanyia kazi, japokuwa mpaka sasa sijaletewa mrejesho wowote na watoto nawaona hapo barabarani," anaeleza Ndipitipi.

**MTENDAJI KATA**

Ofisa Mtendaji Kata ya Kimanzichana, Said Abdalah, anasema tayari walishaanza kufanyia kazi jambo hilo, ikiwamo kukaa na kamati iliyojumuisha vijiji vyote vilivyo katika kata, kupanga mikakati namna ya kulimaliza hilo.

"Katika vijiji vyote vilivyopo katika Kata hii ya Kimanzichana, kijiji hiki ndiko yalipo makao makuu ya Kata na ndicho kimechangamka zaidi na chenye mwingiliano mkubwa wa watu. Kwa hiyo, watoto wengi huwa wanatoka kwenye vijiji vyao na kuja kufanya biashara hizo hapa.

"Baada ya kuona hali inazidi kuwa mbaya na idadi ya watoto wanaofanya hizi biashara za ujasiriamali inazidi kuongezeka, tuliitisha mkutano na viongozi wa vijiji vyote na tukapanga mikakati mbalimbali ya kukomesha hili, ikiwamo kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi cha hapa Kimanzichana, ili waje wawakamate," anasema

Ofisa Mtendaji Kata anataja changamoto kubwa zinazokwamisha mikakati waliowekea ya kumaliza tatizo hizo, ni lawama za wazazi na walezi wa watoto hao, ambao pia wanawanyima ushirikiano.

"Kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi la hapa Kimanzichana, tulikuwa tunafanya 'ambush' (uvamizi) ya kuwakamata watoto, tukiwaambia kwamba ili tuwaachie ni lazima watuhakikishie wanaacha hizi biashara na wanaenda shule. Lakini, tulikuwa tunapata lawama kubwa kutoka kwa walezi na wazazi wao.

"Siku moja tuliwajaza pale Kituo cha Polisi cha Kimanzichana. Walikuja wazazi kwa fujo na wengine walikuwa wanalia, wanasema 'kwanini tunawaweka ndani' wakati hao ndiyo wanawategemea kwa ajili ya kuwatafutia riziki.

"Wao hawana nguvu za kuwatafutia chakula. Yaani unakuta anakuja bibi 'amechoka' analia na machozi mbele ya askari hata unashindwa umfanyeje yule mzee. Kwa hiyo tunahitaji ushirikiano wa wazazi," anasema

**OFISA USTAWI/POLISI**

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Mkuranga, Peter Nambunga, anasema kinachochangia watoto wengi kujiingiza katika kibiashara hiyo ni umasikini uliokithiri.

Pia, anasema uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa elimu kutoka kwa wakazi wengi; ndoa nyingi kuvunjika na wazazi kutokuwajibika ipasavyo katika malezi ya watoto wao.

Polisi kupitioa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Mkuranga(OCID), wanasema bado hawana taarifa hizo, katika ofisi yake na kwamba analifanyia kazi.

## BIASHARA KATIKA PICHA



Mchuuzi wa matikiti akiwahudumia wateja wake, katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma mapema wiki hii. Kipande kimoja cha tikiti kiliuzwa kwa bei ya 500/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Wachuuzi wa miwa wakiwa wamepaki baiskeli zao kusubiri wateja huku kukiwa na jua kali bila kuwa na kitu cha kujikinga katika eneo la Kizuiani Mbagala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wakifanyia shughuli zao katikati ya barabara za mitaa ya eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha usumbufu kwa watembea kwa miguu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UCHUMI

Na Mwandishi Wetu

# Unataka kuchukua mkopo? Pata darasa kamili uchukue uamuzi



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Abdurazak Badru .

KUNA nadharia kutoka kwa wasomi wa uchumi kuhusiana na dhana 'mkopo' au 'ukopoaji.'

Tafsiri yake katika mazingira ya kawaida ni fedha ambazo mtu, asasi au hata serikali inapewa kwa kutimiza malengo maalum na ulopaji wake una kipindi na taratibu maalum.

Mtoaji anaweza kuwa mtu mmoja au kikundi, asasi na serikali, inayoidhinishwa kwa masharti mahsusi katika namna ya kupata pesa hizo na urejeshaji wake.

Kuna taasisi ambazo zimejikita katika biashara hizo, zikiwamo benki, ushirika wa kuweka na kukopa (saccos) na taasisi za kifedha.

Anayepata mkopo, huwa na deni analofaa kulilipa kulingana na makubaliano rasmi yake na anayemkopesha. Deni hilo linaweza kuwa mikopo isiyokuwa na riba au wenye riba.

AINA ZAKE

Kuna aina nyingi za mikopo, kulingana na yanayohitajika na upatikanaji wake unaweza kulingana na ulivyo mkopo wenyewe, anayelengwa na ule mkopo au lengo la matumizi ya ule mkopo.

Mara nyingi utaratibu wake, mkopaji haruhusiwi kwa mwingine, mpaka akamilishe wa kwanza, ingawa kuna mwingine unaoitwa mkopo endelevu, unaoidhinishwa kuchukuliwa, kabla uliotangulia kukamilishwa.

Kuna, mikopo kwa kadri mahitaji yalivyo na anyekopa anakuwa na ama dhamana au kudhaminiwa, mathala kutoka benki na asasi za fedha kama saccos.

Ipo mikopo isiyo na dhamana, mathalan iliyozoeleka kutoka kwa marafiki na jamaa.

Aina za mikopo kulingana na lengo la matumizi, mathalan ujenzi, biashara, kilimo, masomo na ununuzi wa chombo cha usafiri

Ipo mikopo mahsusi kwa ajili ya kulipa mkopo mwingine, ambayo hujulikana kama 'consolidation loan'; na mkopo kukabili dharura ya papo kwa hapo, mathalan matibabu.

Kuna aina za mikopo kulingana na mlengwa alikosimamia, mathalan mahsusi kwa wafanyakazi wa kati au walimu, askari, wakulima na wanafunzi kama ilivyo kwa wanaosoma elimu ya juu nchini.

Mkopo kwa serikali; hiyo inailenga serikali na mara nyingi riba zake huwa nafuu, kama nchi tajiri inavyokopesha mataifa yenye uchumi wa chini.

Pia, kuna mikopo iliyopunguzwa riba, hujulikana kitaalamu kama 'subsidized loan' mara nyingi kwa kundi maalum kama vile serikali na wanafunzi.

**ULIPAJI MIKOPO.**

Mkopo ni deni linalolipwa kulingana na mkataba kati ya anayekopa na anyekopesha. Ikiwa ni mkopo karadha aliyekopa hulipa pesa alizokopa pekee, lakini mkopo wa riba hulipwa kilichotolewa na riba.

Malipo yake hufanyika katika kipindi cha makubaliano na kiwango maaluma kilichopangwa, mathalan siku, wiki au mwezi katika baadhi ya mikataba, ucheleweshaji huendana na adhabu za riba, kuligana na miongozo waliokubaliana, mkopaji na mkopeshaji.

Katika baadhi ya nchi, kuna mashirika yanayowasaidia watu kutumia na kulipa mikopo yao kwa busara.

**KUNA UNYANYASAJI?**

Dhana ya mikopo kwa nia isiyo nzuri, kama vile malipo ya riba, inaangukia katika unyanyasaji kwenye mikopo. Ni dhana ambayo imeshazungumziwa katika lugha ya kukemea kutoka mamlaka za kiserikali nchini.

Vilevile, katika kupeana mikopo, iwapo inatokea hakuna mamlaka inayodhibiti na mwenendo wa mkopo huo, nayo inaangukia katika sura nyingine au kunyanyasa. Nchini, kuna Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Pia, kuna unyanyasaji wa wanaokopa kwa kutolipa deni walilokopa.

**VIGEZO VYAKE**

Kuna vitu vingi vinatajwa ni vya kuzingatia wakati wa kuchukua mkopo, ikaangukia katika sura ya maswali: Kiasi unachohitaji; utalipaje; kama una kipato cha uhakika kumudu marejesho; kumbukumbu za kuambatanisha mchakato wote.

Mkopaji anatakiwa kufanyia kazi kujua ni kiasi gani taasisi ya fedha husika inaaminika, namna bidhaa au sera maalum za mkopo zinazoendana na mahitaji ya mkopaji kama vile sera kwa ajili ya

> **Vilevile, katika kupeana mikopo, iwapo inatokea hakuna mamlaka inayodhibiti na mwenendo wa mkopo huo, nayo inaangukia katika sura nyingine au kunyanyasa. Nchini, kuna Benki Kuu ya Tanzania (BoT).**




Tukio la benki kuzindua aina mojawapo ya mkopo.

UCHUMI

# Unataka kuchukua mkopo? Pata darasa kamili uchukue uamuzi

wanawake, vijana ya wakulima.

Swali lingine, linarejea ni kama mtu ana kipato cha msimu, je ulipaji wake unaweza kupangwa kuendana nalo?

Mkopaji anapaswa kufanyia tathmini riba na gharama gani zingine zilizojificha, katika mchakato wa kupata mkopo au baada ya kuupata huo mkopo.

Lingine la 'kukuna kichwa' inaangukia katika mkopeshaji kama vile benki anahitaji dhamana ya aina gani na namna gani anayekopa anaridhia kuiweka rehani, ili aupate mkopo?

Kutokana maendeleo ya teknoklojia ya sasa, ukosefu wa muda kufanya baadhi ya mambo, unatoa nafasi ya swali kwa baadhi ya wakopaji kama matumizi ya simu yana nafasi katika kurejesha mkopo.

Pia, kuna mustakabali unaoendana na kucheleweshwa mchango na kama kuna adhabu ya aina yoyote?

**KUKWAMA MALIPO**

Kunatajwa kuwapo mengi yanayokwamisha maliopo ya deni la mkopo na katika baadhi ya vigezo, benki zinaweka bima mahsusi kwa mikopo hiyo.

Baadhi ya vigezo vinavyoingia katika orodha inayotajwa, inajumuisha masuala kama, kupoteza kazi kwa mlipaji deni, kunamfanya ashindwe kuhudumia deni analopaswa kudaiwa.

Pia, kuna magonjwa, ikimaanisha mlipaji deni anaopugua, kuna uhusiano wa karibu na uwezekano wake kulipa deni katika namna sahihi au kushidwa kabisa.

Sababu kuu hapo, ni nguvukazi inayotarajiwa kuingiza kipato, inafifia na wakati huohuo, huenda anaingia gharama za ziada nje ya bajeti ya kawaida, kwa ajili ya kujitibu.

Tatu kuna suala la kiwango cha thamani ya fedha, iwe ya kigeni au ya nchini, inamgusa mlipaji kulingana na nafasi yake. Pale anapotegemea fedha za kigeni kulipa deni inaanguka thamani, inamhusu mlipaji kuyumba kimapato.

Vivyo hivyo, katika suala la fedha nyumbani kuangukia thamani kupita kiasi, kunagusa uwezo wa mlipaji kulipa deni, mfano hai ni thamani ya pesa za Zimbabwe, ilipotokea kuanguka kupita kiasi.

Kifo cha mmoja wa wanafamilia wa mlipaji deni, kuna uhusiano wa moja kwa moja na kuyumba kwa bajeti ya mlipa deni na si ajabu, akashindwa kumudu ratiba ya ulipaji deni lake, kama alivyokubaliana katika mkataba. Hiyo inaendana na kupoteza kazi kwa mwanafamilia.

Mwisho, kuna kuibuka matatizo mengine ya maisha, yanayosababisha hasara za kifedha kwa mlipa deni.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Prof. Florens Luoga; msimamizi mkuu wa taasisi zinazokopesha. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**"Mkopaji anapaswa kufanyia tathmini riba na gharama gani zingine zilizojificha, katika mchakato wa kupata mkopo au baada ya kuupata huo mkopo.**

**USIPILIPE DENI**

Ikishafika hatua sura ya rasmi mlipaji anashindwa kulipa, kuna aina ya mchakato wa kufuatiliwa unaanza kutoka kwa mdai, kama vile benki.

Huanza katika sura ya wito wa swali la mdomo 'vipi deni letu?' Kutoka kwa wafanyakazi wa benki wa taasisi ya fedha kumfuata, kisha barua rasmi ya malalamiko kutoka benki usimamizi wa taasisi ya fedha.

Hatua ya juu ambayo ni mbaya zaidi ni utekelezaji wa hatua za kisheria iliyopo kwenye mkataba. Wafanyakazi wa taasisi ya fedha wanaonekana kwenye anwani ya makazi ya mdaiwa, kutekeleza kisheria, azma iliyomo kwenye mkataba.

Ni hapo inashuhudiwa vitisho na amri kutoka huduma maalum za kisheria. Hapo ndipo wenye dhamira nzuri, wanakuja na " kulipa mkopo kwa mkopo." Kama wanamudu vigezo na masharti ya huko, wanakuwa wamejinusuru.



Kupitia nyenzo ya ukopaji, aliyekumbwa madhila ya kutomaliza deni la kwanza, ana nafasi ya kuondosha sekeseke ya deni la awali, anapokidhi vigezo na masharti.

Kupata aina yoyote ya mkopo ni rahisi kwa sababu idadi kubwa ya mipango ya mikopo ni mawazo kupitia sekta ya benki, ambazo zinahuduma za kusaidia kutatua matatizo yanayoambatana.

**'MKOPO KWA MKOPO'**

- Inasaidia wateja wa taasisi za fedha, kuondokana na matatizo ya utumwa na fedha, makosa sahihi yaliyo tolewa mapema.
- Kuna fursa za kulipa mkopo kwa kuongeze wa muda wa kulipa bila ya kupoteza fedha ya uhuru wa kisheria.
- Haina ongezeko la faini na adhabu kwa ajili ya kulipa.
- Malipo yake husaidia kuepuka madai, ambayo yanahitaji muda mrefu na kero.
- Kabla ya kulipa mkopo kwa mkopo, kuna fursa ya kuchagua benki au taasisi sahihi.

**MALIPO YA AWALI**

Malipo ya awali ya mkopo yana faida nyingi. Kwanza, inaelezwa inashughulikia hali ya kisaikolojia ya mdaiwa. Wakati kiasi kilichokopwa kikamilifu, mtu huhisi vizuri zaidi na huru.

Ikiwa anachambua malipo, malipo ya awali ya mkopo kwa moja kwa moja hupunguza kiasi cha madeni kuu ya akopaye kwa kupunguza kiwango cha maslahi yaliyoongezeka.

Malipo ya awali ya mkopo mara nyingi ni ya manufaa kwa wateja, lakini si kwa taasisi za benki. Wanapoteza riba isiyolipwa kwa mikopo juu ya kulipa mapema.

BIASHARA




Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni ya Nas, Prof. Costa Mahalu (mwenye suti nyeusi), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mtendaji wa TTB, Devota Mdachi, baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano kati yao, na kutangaza vivutio vya utalii vya nchi katika viwanja vya ndege duniani. Wanaoshuhudia, kushoto ni Meneja Mkuu wa Nas, Miguel Serra na kulia, Mwenyekiti wa TTB, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

MKATABA TTB & NAS...

# Utalii nchini 'kupaishwa' vivutio viwanja vya ndege kibao duniani

- Prof. Mahalu adokeza mazito yajayo
- Mikumi, Serengeti sasa kila mahali
- Jaji Mihayo: Hii hapa Safari ya utalii

**Na Beatrice Philemon**

TANZANIA ni kati ya nchi chache duniani zenye vivutio bora na vingi vya utalii. Ni bahati mbaya havijajulikana kwa kiwango kinachostahili kimataifa.

Ni walakini uliokwishabainika na umeanza kufanyiwa juhudi za kufanikisha lengo la kuwezesha kujulikana huko. Hatua mojawapo, ni Kampuni ya Huduma za Usafiri wa Anga (Nas) imeingia mkataba wa makubaliano (MOU) na Bodi ya Utalii wa Tanzania (TTB) kutangaza vivutio vya utalii nchini.

Nas itafanya kazi hiyo katika viwanja vya ndege mbalimbali duniani, kwa matarajio ya kusaidia vivutio vya utalii vya Tanzania kimataifa, vitakayoongeza watalii wanaofika nchini, ikiendana na kuingizia nchi fedha za kigeni na wawekezaji katika sekta ya utalii.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini mkataba huo, Mwenyeki wa Bodi ya Kampuni ya Nas, Prof. Costa Mahalu, anasema katika utekelezaji, kampuni yake kwa kushirikiana na TTB kutangaza utalii katika kumbi za wasafiri katika viwanja vya ndege duniani.

Anasema, ni fursa inayotajwa itawawezesha wasafiri wanaopumzika wa watambue vivutio vya kitalii vilivyopo nchini. Prof. Mahalu anafafanua: "Katika 'lounges' kutakuwepo matangazo na vijarida mbalimbali vinavyotangaza utalii wa hapa nchini, ili kuamsha ari na hamu ya kutembelea vivutio vya utalii."

Kuhusu undani wa malengo ya ushirikiano, anasema ni kuwawezesha kupatikana taarifa zinazohusu utalii wa Tanzania na kuwapatia abiria wanaopita 'lounges' zinazoendeshwa na Nas wakiwa safari.

Anataja baadhi ya maeneo yanayonufaika na matangazo hayo ni viwanja vya ndege vya Afrika kama vile nchini Rwanda, Msumbiji, Morocco, Misri na Cote D'Ivoire, vivyo hivyo Mashariki ya Kati na Asia, watakapobadilishana maarifa kuboresha taswira ya utalii Tanzania.

Kwa mujibu wa Prof. Mahalu, kampuni ya Nas ilianza biashara nchini kupitia kampuni yake tanzu ya Nas - Dar Airco mwaka 2016. Hilom analifafanua akisema: "Takwimu za mwaka 2019 mpaka sasa, zinaonyesha kampuni imehudumia ndege 8,900."

Anasema ubora wa utoaji wa huduma zake au kitaalamu 'on time performance - OTP' uko juu, kampuni hiyo imeajiri wafanyakazi 364 na ina mitambo na vifaa vya kufanyia kazi, huku ikiendelea kuwekeza vifaa, mitambo na mafunzo kwa wafanyakazi.

Pia, anasema kimataifa imeajiri wafanyakazi zaidi ya 8000 kutoka katika nchi tofauti duniani na Prof. Mahalu anaeleza: "Kampuni inaamini Tanzania ni nchi inayofaa kuendelea kuwekeza kutokana na mazingira mazuri ya kibiashara, amani na utulivu uliopo nchini."

MKATABA ULIKOSIMAMA

Prof. Mahalu anataka maeneo matatu ya huduma za mkataba ni kutangaza utalii wa ndani na nje ya nchi katika viwanja vya ndege, inayotekelezwa kwa ushirikiano wake na TTB."

> "Tunashirikiana na taasisi mbalimbali kama Chuo cha Taifa chaUsafirishaji (NIT) na vyuo vya elimu ya juu, kuwafundisha vijana wanaomaliza, chini ya programu yetu ya mafunzo kazini yaani 'internship,'' anasema

Anataja eneo la pili, ni afya kwa jamii ambayo kwa sasa kampuni inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na la tatu ni sekta ya elimu.

"Tunashirikiana na taasisi mbalimbali kama Chuo cha Taifa chaUsafirishaji (NIT) na vyuo vya elimu ya juu, kuwafundisha vijana wanaomaliza, chini ya programu yetu ya mafunzo kazini yaani 'internship," anasema

Kwa mujibu wa Profesa Mahalu, programu ya mafunzo kazini ilianza jijini Dar es Salaam tangu mwaka 2018 na iliendelea katika mikoa mingine kama Kilimanjaro na Dodoma .

Anasema, asilimia 10 ya wanafunzi wanaochukuliwa katika mpango huo wa mafunzo kazini, walipatiwa mikataba ya ajira.

**WIZARA UTALII**

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji Mstaafu, Thomas Mihayo, anasema makubaliano kati ya TTB na Nas, imo katika mbinu mpya ambazo bodi imeingia mkataba kutangaza utalii kuwa kivutio bora cha Afrika na hata duniani.

"Hatuwezi kuingia 'MOU' bila ya kufanyia uchunguzi. Nimefurahi Nas imetimiza vigezo ambavyo vinatakiwa katika sekta ya utalii," anasema Jaji.

"Naomba wakala wa wasafirishaji watalii na wadau wengine waliopo katika sekta ya utalii, watumie fursa hii kuandaa historia ya kampuni zao (company profile), huduma za utalii wanazozitoa, bei wanazotoza kutembelea vivutio vya utalii na masuala mengine na kuziletea kampuni ya Nas," anasema.

Jaji Mstaafu Mihayo anaongeza: "Watalii wakija waone 'package' zao na huduma wanazotoa, ili wakiamua kutembelea Tanzania, wawe wamejipanga vizuri."

Anatamba kwamba, TTB imejipanga vizuri kutumia fursa iliyopo katika kutangaza vivutio vyote katika viwanja 17 vinavyo hudumiwa na kampuni ya Nas.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kingwangalla, anaisifu sekta ya utalii ni muhimu sana nchini na sekta hiyo inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 17 .6 na robo ya fedha zote za kigeni nchini.

Kwa mujibu wa wizara mama ni sekta inayotoa ajira za moja kwa moja 600,000 na nyinginezo zaidi ya milioni mbili.

"Ili sekta ya utalii iweze kukua na kutimiza lengo linalokusudiwa, lazima tuwe na uwekezaji nchini na ndiyo maana tumefufua shirika letu la ndege (ATCL) ili kurahisisha usafiri kwa watali wanaokuja kutembelea Tanzania," Dk. Kigwangalla anafafanua akisema, sehemu kubwa ya abiria ni watalii.

"Ifikapo 2025 tunaweza kupata Sh. bilioni 16 kama tutawekeza zaidi na lazima tuwe wabunifu namna ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii na namna ya kufikia watalii," anasema

Hivi sasa Tanzania imeanza kutafuta watalii katika nchi za Asia, China, Russia na inajiandaa na ghuba ya Uarabuni na Mashariki ya Kati na waziri anahimiza sekta na hasa wakala katika biashara ya utalii, wanapaswa kuwa wabunifu zaidi katika utoaji huduma zao.

"Naipongeza TTB na Nas kuingia mkataba wa makubaliano na kutupa viwanja 40 vya ndege, ambavyo wanavitumia bila ya gharama yoyote kutangaza vivutio vyetu vya utalii, pia kusaidia kutengeneza matangazo ya kuweka kwenye hayo mabasi na serikali itaendelea kutoa msaada inavyotakiwa," anasema Dk. Kigwangwala.

Anaeleza matarajio ya mkataba huo ni kuleta matokeo chanya na kuhamasisha wageni kutembelea Tanzania, zaidi, badala ya kuishia kwenye picha na matangazo.



Mandhari ya baadhi ya vivutio vya nchini vinavyotarajiwa kuonyeshwa kimataifa. **PICHA: MTANDAO.**



# Waliompopoa DC mawe wafurahia Tasaf

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAKAZI wa Kijiji cha Mpunguti katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuendelea kusaidia kuinua uchumi wao kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf). Wananchi wa Kijiji hicho ndio waliouvamia msafara wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo na 'kuupopoa' na mawe mwaka jana kutokana na kuzuiliwa kuwaua baadhi ya wanafamilia, ambao walikuwa wanawatuhumu kwa ushirikina.

Kwenye tukio hilo, magari kadhaa ya serikali yaliharibiwa vibaya, ndipo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipoagiza Jeshi la Polisi kuwashushia kipigo usiku kucha, tukio ambalo liliwafanya wajutie kile walichokifanya.

Wakizungumza juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, baadhi yao waliishukuru serikali kuwasamehe kutokana na unyama walioufanya na kuendelea kuwa miongoni mwa vijiji vinavyonufaika na Tasaf. Walidai kupitia mpango wa Tasaf, baadhi ya familia zinazonufaika zimeboresha makazi, kuanzisha shughuli za uzalishaji ikiwamo kilimo, ufugaji na biashara ndogo ndogo.

Mmoja wa wanufaika, Ambangile Mwaibabile, alisema kabla hajaanza kunufaika na mfuko huo maisha yake yalikuwa magumu na hakuwa na uwezo wa kujenga nyumba nzuri ya kuishi, lakini sasa amejenga nyumba nzuri ya kuishi na familia yake.

Alisema fedha alizopata awali alizitumia kukodi mashamba kwa ajili ya kulima mpunga na baada ya kuvuna, aliuza akanunua bati akahifadhi, awamu ya pili akanunua tofali na kuanza kujenga nyumba ambayo kwa sasa imekamilika. "Tunaishukuru serikali ambayo pamoja na mabaya yetu katika hiki kijiji, lakini inaendelea kutukumbuka, tulikuwa na maisha magumu kupita maelezo, lakini kwa sasa hali ni nzuri."

Naye Nelusigwe Ambokile, alisema pamoja na kwamba mpango huo umemnufaisha yeye pamoja na familia yake, lakini anaiomba serikali kuwasaidia na wengine katika kijiji hicho ambao wanastahili kusaidiwa, lakini hawakuingizwa kwenye mpango.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Kaini Mwampepe, alisema tangu mwaka 2015 mpaka sasa wananchi wa kijiji hicho wanaonufaika na mpango huo ni 84 na kwamba fedha zilizotumika ni Sh. milioni 58.

Alisema awali zilibainika kaya 98, lakini baada ya mchujo zikaondolewa kaya 10 kutokana na kukosa sifa, hivyo zikabakia kaya 88 na kutokana na sababu mbalimbali zimepungua tena.

Mwanjelwa aliwahakikishia wananchi hao kuwa serikali itaendelea kutekeleza mpango huo, na kwamba katika Tasaf awamu ya tatu sehemu ya pili, vijiji vyote ambavyo havikuwamo kwenye mpango vitaingizwa.

Alisema hata kaya ambazo zinakidhi vigezo vya kuingia kwenye mpango, lakini katika awamu zilizopita hazikuwamo, zitaingizwa ili nazo zinufaike na kwamba wanufaika wa awali ambao wataonekana kuwa wameondokana na umaskini, wataondolewa kwenye mpango."

"Mheshimiwa Rais anawapenda wananchi wake na ndio maana ameuzindua upya mpango huu, na kwa wale mliokuwa mnafuatilia wakati anazindua alitupatia maelekezo ya kuboresha na tutafanya hivyo, wanufaika tumieni vizuri fedha hizo," alisema Mwanjelwa.

# Vijiji 140 vyapata umeme wa REA

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

VIJIJI 140 vimefanikiwa kuwashwa umeme mkoani Mbeya katika utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini (REA) awamu ya tatu katika mzunguko wa kwanza ambao umetekelezwa ndani ya miezi 24.

Kauli hiyo ilitolewa na Mhandisi wa Rea Mkoa wa Mbeya, Yolam Mtemi, na kuweka wazi kuwa utekelezaji wa mradi huo umefanikiwa kwa wakati licha ya makubaliano ya mkataba ambayo yatatarajia kukamilika Aprili 10, mwaka huu.

Alisema utekelezaji wa mradi huo unajumuisha njia kuu za umeme zinazofikia urefu wa kilomita 331.47 na njia ndogo ya umeme yenye urefu wa kilomita 573.34

Alisema katika mchanganuo, Halmashauri ya Mbeya Vijijini kuna jumla ya vijiji 30 vilivyowashwa umeme, vijiji 22 katika Halmashauri ya Rugwe, vijiji 42 katika Halmashauri ya Busokelo na vijiji 22 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

Mtemi alivitaja vijiji vingine vilivyowashwa katika mradi huo ni 10 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na 13 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na kuwa katika uwashaji umeme kwa vijiji hivyo 140 inajumuisha transfoma 168.

"Utekelezaji wa mradi huu wa Rea katika mzunguko wa kwanza umefanikiwa kwa asilimia 100 na ndiyo maana kuna vijiji 140 ambavyo vimewashwa umeme katika halmashauri hizo.

Alifafanua kuwa katika mradi huo jumla ya wateja 7,549 wa njia ndogo wameunganishwa na wateja 157 kati ya 817 wa njia kubwa wameunganishwa na kuwa hatua za utekelezaji zinaendelea kukamilisha wateja wote.

Alisema katika mradi huo kwa mujibu wa mkataba ni lazima kuwapo na nyongeza ya asilimia 15 ya vijiji ambapo katika utekelezaji wake kuna jumla ya vijiji 19 vitaunganishwa ndani ya muda wa mkataba wa Rea awamu ya tatu katika mzunguko wa kwanza.

Mtemi alisema katika utekelezaji huo, Halmashauri ya Mbeya vijijini itanufaika kutokana na kupata vijiji 14 kati ya 19, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe vijiji 3 kati ya vijiji hivyo 19, Halmashauri ya Busokero kijiji kimoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kijiji kimoja.

Alisema katika utekelezaji wa nyongeza ya vijiji 19 vinavyotokana na asilimia 15 ya vijiji kuna jumla ya transfoma 25 zitakazofungwa katika vijiji hivyo na kuwa ufungaji huo ni sawa Km 39.09 kwa njia kuu na Km 102 .02 kwa njia ndogo.



Mmoja wa wanufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), Ambangile Mwaibabile (aliyepiga magoti), mkazi wa Kijiji cha Mpunguti, wilayani Kyela, akimkumbatia Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alipomtembelea nyumbani kwake kukagua nyumba aliyoijenga kwa kutumia fedha anazopata kupitia mpango huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wafanyabiashara ya asali wapewa somo vifungashio

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa asali wametakiwa kuzingatia ubora wa vifungashio vya bidhaa za asali kwa lengo la kuimarisha ushindani katika soko kwa kuwa vifungashio visiyo na ubora vimekuwa vikichangia bidhaa hiyo kushindwa kustawi na kupunguza ubora.

Kauli hiyo imetolewa jana na Ofisa Nyuki Mkoa wa Mbeya, Marietha Kereti, wakati akizungumza na gazeti hili na kubainisha kuwa maofisa nyuki hulazimika kufanya msako mtaani kwa lengo la kuwabaini wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiuza bidhaa ya asali bila vifungashio bora.

Alisema kumekuwapo na kasumba ya baadhi ya wafanyabiashara wa asali ambao wamekuwa wakiokota makopo, ambayo yametumika kwa shughuli nyingine na kuyatumia kuhifadhia asali na kasha kuwauzia wateja malimbali.

"Makopo, chupa au ndoo zilizotumika kuhifadhia bidhaa zingine hazifai hata kidogo kuhifadhi asali kwa kuwa asali inatabia ya kufyonza uchafu wote katika kifaa kilichotumika na hivyo kupoteza ubora kwa ajili ya matumizi ya binadamu," alisema.

Alisema umefika wakati kwa wauzaji wa asali kutumia vifungashio bora kwa lengo la kukuza biashara ya asali na kuongeza ushindani wa kibiashara na mataifa mengine duniani.

Marietha alisema vifungashio visivyokidhi ubora vimekuwa vikisababisha mahitaji ya soko la asali katika jamii kupungua kutokana na wengi wa wateja kuhofia mazingira ya biashara ya asali katika soko.

Aidha, alisema katika mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Chunya ndiyo wilaya pekee inayoongoza kwa uzalishaji wa asali, kutokana na maeneo mengi ya wilaya hiyo kuwa rafiki katika ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa asali ya kutosha.

Alisema hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2019 mkoa wa Mbeya ulikuwa na jumla ya mizinga ya asili 54,548 na mizinga ya kisasa 8,363,na kuwa bado kuna mpango endelevu wa kuwaelimisha wafugaji wa nyuki kutumia mizinga ya kisasa kwa lengo la kuongeza ubora wa uzalishaji.





# Apiga 'stop' ulazaji nguzo barabarani

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewaonya makandarasi wanaotelekeza miradi ya umeme vijijini kuhusu kulaza ovyo nguzo za umeme barabarani kwa muda mrefu bila kusimikwa.

Alitoa onyo hilo juzi alipowasha umeme katika Kata ya Farkwa wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Waziri Kalemani alisema ameshuhudia kuzagaa kwa nguzo barabarani, jambo ambalo linamkera na kuagiza makandarasi hao kuacha tabia hiyo kwa kuwa inasababisha nguzo kuoza kabla ya kutumika.

"Kuna shida moja na nitoe onyo la mwisho, nimepita barabarani nguzo zimelala, Meneja wa Kanda na Mkoa simamia haya, nimetoa siku tatu kwa nguzo zote zilizolala kwenye mkoa wote wa Dodoma ziondolewe, tofauti na hivyo mhandisi uache kazi na wewe mkandarasi tutakuandikia barua ya kusitisha mkataba wako," alionya.

Alimwagiza Meneja wa Mkoa wa Dodoma kusimamia suala hilo na kumtaka kumwandikia barua mkandarasi atakayeshindwa kusimamia suala hilo. "Hatuwezi kuacha fedha ya serikali ikichezewa kwa kuacha nguzo ziendelee kuoza, hili ni onyo la mwisho na ni onyo kwa makandarasi wote nchi nzima, ni marufuku nguzo kulazwa chini, zikifika ndani ya siku tatu zisimikwe wananchi wapate umeme," aliagiza. Waziri huyo pia alisema serikali imetoa Sh. bilioni 40.2 kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye vijiji mbalimbali nchini.

"Kila mwananchi hivi sasa anapaswa kuwa na umeme kutokana na kwamba maendeleo hayaji bila kuwa na umeme, ni jambo jema kuona kila kijiji kinakuwa na umeme, wananchi mtumie vizuri umeme huu," alisema.

Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia (CCM), alisema umeme huo utasaidia kubadilisha maisha yao ya kila siku, akitamba kuwa watu watafanya biashara ili kujiongezea kipato.

"Wananchi acheni kusikiliza maneno ya uongo fanyeni kazi ya kujiletea maendeleo," alisema. Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, alisema kuwashwa kwa umeme Farkwa kumechangia kuongeza maendeleo katika eneo hilo.

Odunga alisema wananchi wengi wanafanya biashara, hivyo umeme utawaongezea upanuzi wa biashara wanazofanya. "Tunaishukuru serikali kwa kuleta umeme vimebaki vijiji vichache kukamilisha vijiji vingine kuwa na umeme," alisema.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mwalimu Queen Mlozi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, akitoa wito kwa wanawake wote nchini, kujitokeza kushiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Dunia Machi 8 mwaka huu, na kushiriki kufanya shughuli za kijamii kwenye maeneo yao ili kuienzi siku hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake waitwa fursa uongozi CWT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Idara ya Jinsia na Wanawake ya Chama cha Walimu (CWT), Stella Mamotto, amewataka wanawake kuchangamkia fursa katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho.

Akizungumza katika kikao cha baraza la chama hicho Mkoa wa Dodoma jijini hapa juzi, Mamotto alisema mwaka huu chama hicho kina mambo makubwa mawili ambayo ni sherehe za Mei Mosi na uchaguzi mkuu wa viongozi kwa nafasi mbalimbali.

Aliwataka wanawake ndani ya chama hicho kuzingatia usawa kwa nafasi zote zitakazogombewa wakati wa uchaguzi mkuu.

"Kama kinamama wakijitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi, hakika wataweza kuvisemea vikwazo vyao na hata kutatua matatizo ya kinababa kwa ujumla.

"Hivyo, kwenye uchaguzi, kama kuna nafasi sita, basi tuhakikishe nafasi tatu za uongozi ziende kwa kinamama ili kuifikia ile 50 kwa 50.

"Niwatoe hofu tu kinamama wanaotaka kugombea ndani ya CWT, msiogope kugombea, kumbukeni katiba ya chama chetu inavyosema, hakuna mwenye hatimiliki ya nafasi zozote, ukitosha utachaguliwa na utashinda," alihimiza.

Alisema mwanachama yeyote aliye hai, ana haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi ndani ya CWT.

# Waziri aagiza matumizi Tehama sekta ya elimu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, amewataka walimu na wanafunzi kuvitumia vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) vilivyotolewa na serikali na wadau, kujiendeleza kielimu.

Alitoa rai hiyo juzi kwenye uzinduzi wa mradi wa kuunganisha shule 163 nchini na mtandao wa intaneti uliofanyika jijini hapa chini ya usimamizi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kushirikiana na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Vodacom Tanzania.

Kwandikwa aliyataka makundi yaliyopatiwa vifaa hivyo, kuhakikisha yanavitumia kwa kujiendeleza zaidi kimasomo.

"Leo tumezindua rasmi mfumo huu wa mradi wa kuunganisha shule 163 za hapa nchini na mfumo wa intaneti, nimeona kuna vitabu vingi humu kwa kila somo, hivyo tunatakiwa kuutumia mfumo huu kujiongezea elimu," aliagiza.

Naibu Waziri huyo alisema Tehama isitumike kwa kutafuta mambo mabaya kwenye kompyuta hizo kwa kuwa lengo ni kuwasaidia kujifunza zaidi.

Alibanisha kuwa kwenye kompyuta hizo kuna mifumo iliyowekwa kumsaidia mhusika kujifunza masomo mbalimbali ya sayansi.

Alisema uwapo wa vifaa vya kompyuta shuleni, utasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi kupenda kusoma masomo ya sayansi na Tehama.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashimba, alisema mradi huo unatekelezwa na serikali kupitia mfuko huo kwa ushirikiano wa Vodacom Tanzania.

Mashimba alisema uzinduzi mradi huo utaziunganisha shule 163 za mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani kwa mtandao wa intaneti na hiyo ni awamu ya pili ya mradi.

Alisema awamu ya kwanza ya majaribio ya mradi huo ilihusisha mikoa miwili ya Simiyu na Tabora ambayo shule 24 ziliunganishwa na mtandao wa intaneti.

Alisema lengo la mfuko ni kuhakikisha wanafikisha huduma ya mawasiliano maeneo yote ya vijijini ili wananchi wanufaike na huduma ya mawasiliano hayo.

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2014/2015 na hadi sasa, jumla ya shule za umma 558 zimepata vifaa vya Tehama ikiwa ni pamoja na kompyuta tano kwa kila shule na printa moja.

Mkurungenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Hisham Hendi, aliwataka wahusika waliopokea vifaa hivyo, kuhakikisha wanavitunza.

Hendi alisema kampuni yao imetoa kompyuta 806 na viunganishi vya vifaa ya mifumo ya intaneti na shule hizo watatumia kwa mwaka moja bila malipo.

Alisema kampuni hiyo ilifadhili mafunzo kwa walimu wa masomo ya Tehama yaliyotolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuwafundisha wananchi.



## Serikali kuendelea kutatua kero za Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutatua changamoto za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwenye sekta ya habari ili kukuza lugha ya Kiswahili nchini.

Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahamoud Thabit Kombo, alisema hayo katika hafla ya utiaji saini kuhusu ushirikiano wa utendaji wa mambo yasiyo ya Muungano katika wizara zenye dhamana ya mambo ya habari.

Alisema makubaliano hayo yatasaidia matumizi ya ndege zisizo na rubani na upatikanaji wa chaneli ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) katika ving'amuzi vyote nchini bila ya malipo kwa lengo la kuimarisha uhusiano na kukuza lugha ya hiyo nchini.

Alisema makubaliano hayo pia yataendeleza ukuaji wa Kiswahili kimataifa kwa kutoa waandishi wa habari kutoka Tanzania ambao watatumia na kukitangaza Kiswahili katika vyombo hivyo pamoja na uanzishwaji wa vituo vya utamaduni nje ya nchi.

Waziri Kombo alisema wataendeleza kutangaza utalii na utamaduni nje ya nchi na kuimarisha michezo pamoja na kukuza utendaji kwa lengo la kuleta maendeleo nchini.

Alisema jukumu la kufundisha na lugha ya Kiswahili nchini ni la Baraza la Kiswahili Zanzibar (Bakiza) na Baraza la Kiswahili la Tanzania (Bakita), alisema ni vyema kutoa wataalamu wazuri watakao fundisha lugha hiyo ili iweze kukua na kuimarika zaidi.

"Inashangaza sana kumkuta mtu asiye Mtanzania anafundisha Kiswahili nje ya nchi au waajiriwa wasio Watanzania wanaajiriwa kwa kigezo cha lugha ya Kiswahili, mfano wa wazi ni Shirika la Ndege la Kimataifa la Emirates Airline waajiriwa wengi walioajiriwa kwa minajili ya kutumia Kiswahili ni Wakenya na sio Watanzania ni jambo la kushangaza," alisema Waziri Mahamoud.

Waziri wa Habari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Harrison Mwakyembe, alisikitishwa na baadhi ya raia wasio Watanzania kutumia njia hiyo ya lugha ya Kiswahili kupata ajira bila Watanzania wenyewe kufaidika nayo.

# Wizara ya Kilimo yaagizwa kusimamia miche ya karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhakikisha miche ya karafuu inayotolewa na serikali kwa wakulima, iwe imekomaa iweze kukua vizuri.

Aliyasema hayo Ikulu Mjini Zanzibar katika mkutano wa Baraza la tatu la Biashara, ambao ulijadili maazimio yaliofikiwa katika Jukwaa la tisa la Biashara lililofanyika Novemba 21, 2018, mkutano ukilenga kuifahamisha jamii kuhusu makubaliano ya mambo muhimu ya mwenendo wa kibiashara yaliofikiwa kati ya sekta binafsi na serikali.

Alisema ni muhimu kwa wizara hiyo kuhakikisha miche ya mikarafuu inayotolewa na serikali kwa ajili ya kugaiwa wakulima inafikia miaka miwili ili kuondokana na malalamiko ya baadhi ya wakulima kuwa miche mingi hufa baada ya muda mfupi wa kupandikizwa, kwa vile haikuwa imekomaa. Alisema ni muhimu kwa watendaji wanaoshughulikia ugawaji huo, kuhakikisha miche hiyo inawafikia walengwa wa kilimo hicho, ili kuondokana na manung'uniko ya baadhi ya wakulima kukosa miche hiyo.

Aliwataka wananchi, hususan kisiwani Pemba, wenye taarifa za mashamba ya mikarafuu yenye mkanganyiko wa uhalali wake, kutoa taarifa serikalini ili yaweze kufuatiliwa na kutathminiwa.

Dk. Shein aliipongeza Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa kuanza kushughulikia maeneo ya kihistoria na mambo ya kale, hatua inayothibitisha umuhimu wa serikali kuanzisha wizara hiyo. Alisema kuna kazi kubwa na endelevu inayohitaji kufanywa ili kuimarisha sekta ya utalii nchini, kupitia maeneo ya kihistoria na mambo ya kale.

Alisema Zanzibar ina utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii, hivyo hatua ya wizara hiyo kuanza kuviimarisha vivutio vya kihistoria vilivyopo ni ya kutia moyo.

Alieleza umuhimu wa kuwapatia mafunzo watendaji wa wizara hiyo na kuitaka Jumuiya ya Uwekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI) na Jumuiya ya watembeza watalii Zanzibar (ZATO), kushirikiana na serikali kufanikisha azma ya kuimarisha utalii nchini.

Alisema wizara hiyo ina wajibu wa kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali ili kuzitafutia ufumbuzi changamoto katika Sekta ya Utalii, ikiwamo changamoto ya ajira kwa vijana wa Zanzibar. Kuhusu suala la mrundikano wa kontena bandarini, Dk. Shein alisema ujenzi wa bandari mpya ya Mpigaduri ndio suluhisho la tatizo hilo.

Alisema idadi ya wananchi wa Zanzibar imeongezeka na harakati za kimaisha, wakati ukubwa na uwezo wa Bandari ya Malindi umebaki kama ulivyokuwa miaka mingi iliyopita na kusababisha kutokuendana na mahitaji halisi ya wakati uliopo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Ujumbe wa Wafanyabiashara kutoka Nigeria, walipofika Ikulu, mjini Zanzibar jana, wakiongozana na Balozi wa Nigeria nchini Tanzania, Dk. Sahabi Isa Gada (wa pili kulia), kuonana na Rais na kufanya mazungumzo. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Vyama vya siasa vyapewa angalizo wagombea wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VYAMA vya siasa nchini vimetakiwa kufahamu wanawake wanaweza kugombea nafasi mbalimbali kupitia ndani ya vyama na kuongoza katika majimbo na wadi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Akisoma mapendekezo ya wanamtandao wa asasi za kiraia za wanawake kuhusu mwongozo wa Tume ya Maadili ya Vyama vya Siasa kwa uchaguzi mkuu wa 2020, Mwenyekiti wa Mtandao Bahati, Issa Suleiman kwa waandishi wa habari, alisema wakati umefika kwa mwongozo wa Tume ya Maadili wa Vyama vya Siasa kuweka bayana suala la uwapo wa usawa wa kijinsia katika uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa na kuhakikisha kuwa vitendo vyote vya ukatili wa wanawake wakati wa uchaguzi vinapigwa vita.

Alisema imezoeleka wakati wa uchaguzi mwanamke anapogombea, baadhi ya watu humdharau na kumshusha hadhi yake ili aonekane hafai kuwa kiongozi.

Bahati alisema mapendekezo yao kwa mwongozo wa Tume ya maadili ya vyama vya siasa kiwepo kipengele kitakachoweka bayana adhabu kwa atakayethibitika kufanya vitendo vya udhalilishaji wakati wa kampeni na uchaguzi.

Alisema ni muhimu kuweka utaratibu wa kupeleka malalamiko kuhusu vitendo vya ubaguzi na udhalilishaji wakati wa uchaguzi na chombo cha kushughulikia malalamiko hayo ili akitokea mtu anayefanya vitendo hivyo achukuliwe hatua.

Alisema mwaka 2015 kuna vitendo vya udhalilishaji vilitokea ambavyo vilipangwa kwa makusudi hadi kusababisha baadhi ya wagombea wanawake kujitoa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi ikiwamo Mkoa wa Kaskazini Unguja kuwapo na vitisho dhidi ya wanawake.

Alisema hali ya kubezwa na kudharauliwa mwanamke inarudisha nyuma jitihada za usawa wa kijinsia na kutimia maazimio ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (Sadc).

Mwanaharakati kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja ambaye aliwahi kuwa mgombea wa nafasi ya uongozi, Mwanajuma Kassim Makame, alisema katika kipindi cha uchaguzi kuna mambo mengi yanatokea hususan mwanamke anapotangaza nia ya kugombea, hukutwa na changamoto nyingi ikiwamo ya kudhalilishwa.

Aliyekuwa mbunge mwaka 2010 kwa tiketi ya Chadema, Mwanamrisho Taratibu Abama, alisema kipindi cha uchaguzi wanawake wengi hushindwa kufikia ndoto zao za kugombea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kudhalilishwa na kudharauliwa na baadhi ya wanaume.

Alisema kuna matatizo mengi ndani ya vyama vya siasa wakati wa uchaguzi kuhusu nafasi za kugombea kwa wanawake wanapoingia katika jambo na kuomba kura.

# Mafunzo stakabadhi ghalani kuanza

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika nchini, imezindua mafunzo kwa watendaji na wadau muhimu katika kuendesha mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, kwa jamii ya mikunde ya choroko na dengu katika Mkoa wa Mwanza.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Dk. Titus Kamani, alisema juzi katika uzinduzi huo uliofanyika jijini hapa, kuwa mafunzo hayo yamelenga kuboresha usimamizi wa mazao ya wakulima ili waweze kupata bei bora yenye kuwakomboa kiuchumi.

"Mfumo huu upo na umekubalika kitaifa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa ajili ya kuhakikisha kunapatikana bei bora ya wakulima wa mazao hayo mchanganyiko ambayo ni choroko, dengu, soya, ufuta, mbaazi na cocoa," alisema.

"Lengo letu ni kujenga ushirika wa kuaminika na kuondoa udanganyifu wa bei ya mazao ya wakulima, hata wanunuzi watanunua katika maghala yetu kwa ushindani kulingana na bidhaa yenyewe ilivyo na ubora, watashindanishwa mnunuzi atakayetoa bei kubwa ndiye atapewa bidhaa, tumeona Kanda ya Ziwa tuanze na mazao ya choroko na dengu, alisema Dk. Kamani.

Alisema katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Lindi, Ruvuma, Mtwara na Pwani, ulishaanza kutumika na sasa takribani miaka mitatu katika mazao ya soya, mbaazi, ufuta na cocoa inayolimwa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya.

Alisema wakulima watakaonufaika na mfumo huo ni pamoja na mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, kupitia vyama vya msingi vya ushirika vya mazao (Amcos), vitafanya kazi ya ukusanyaji wa mazao hayo na kuyaweka ghalani, chini ya usimamizi mkuu wa chama kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU) ili wanunuzi binafsi waje kununua kupitia mfumo huo.

Alisema kuwa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani utasaidia kuwaunganisha wakulima moja kwa moja pamoja, katika uuzaji wa mzao yao na kupata bei kubwa tofauti na mfumo wa ulanguzi unaotumika kutoka kwa wanunuzi binafsi wanaotumia mizani isiyokuwa na vipimo vya wakala wa vipimo, alisema Dk. Kamani.

Alisema, kutokana na uelewa mdogo wa wakulima wanauza mazao yao kiholela kwa walanguzi bila kutumia mizani na wakati mwingine huuzia shambani na kujikuta wakipunjwa.

Kwa upande wake Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Charles Malunde, alisema wakati wa kuuza mazao hayo, watakuwa wakitangaza kwenye mitandao ya kijamii na kwamba hivi sasa mwezi huu wa Machi 2020, watauza mazao hayo kwa njia ya mnada yatakayokuwa yamekusanywa kwenye maghala husika.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Insignia Ltd ambao ni watengenezaji wa rangi za Coral & Galaxy Paint, Kisan Dhebar (katikati), akihojiwa na vyombo vya habari wakati akizungumzia maadhimisho ya miaka 30 ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Ofisa Masoko wa Insignia, Julieth Mdegela. **MPIGAPICHA WETU**

# Msako waliokaidi kwenda sekondari kuanza

**Na Gurian Adolf,**
TANGANYIKA

JUMLA ya wanafunzi 300, sawa na vyumba saba vya madarasa vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 45 kila kimoja, hawajaripoti shuleni tangu walipochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Kutokana na hali hiyo Mkuu wa wilaya hiyo, ameamua kutangaza operesheni maalumu itakayofanyika nyumba hadi nyumba kwa lengo la kuwasaka wanafunzi hao pamoja na wazazi wao ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria kujibu tuhuma kuhusiana na kitendo cha wanafunzi hao kuto ripoti shuleni.

Alisema serikali imeamua kutoa elimu bila malipo, lakini kuna baadhi ya wanafunzi hawaoni umuhimu wa elimu, na wazazi wao wakikaa kimya, kitendo ambacho kinaashiria kuwa wanaunga mkono makosa ya watoto wao hivyo serikali imeamua kuwajibika kwa kuwachukulia hatua.

Mkuu huyo wa wilaya alisema utafanyika msako wa nyumba kwa nyumba ukiwahusisha watendaji wa serikali, viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya vitongoji hadi wilaya ili kuhakikisha wanafunzi hao wote wanakamatwa na kufikishwa mahakamani.

"Hatuwezi kukubali wanafunzi wote hawa wakashindwa kuendelea na elimu ya sekondari, tena pasipo sababu zozote...ni lazima watafutwe wao na wazazi wao wafikishwe mahakamani ili wajibu tuhuma, kwani hali hii ni lazima ikomeshwa na ni lazima watoto hawa wasome," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Rojas Rumuli, alisema halmashauri imeshakamilisha miundombinu ya shule zote za sekondari hivyo hakuna sababu ya msingi ya kumfanya mzazi ashindwe kumpeleka mtoto wake shule.

## BancABC yaibuka kidedea tuzo ya visa

**Na Romana Mallya**

BENKI ya BancABC Tanzania imeshinda tuzo ya Visa maarufu kama "Visa E-commerce Issuing Growth Award" kutokana na huduma zake za malipo ya mtandaoni ambazo ni nafuu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam baada ya kupokea tuzo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC Tanzania, Imani John, alisema wanajisikia fahari kushinda kwenye soko ambalo lina ushindani mkubwa.

"Hii inaonyesha ni namna tumejizatiti kuhakikisha tunawarahisishia wateja wetu kufanya miamala yao mbalimbali," alisema.

John alisema BancABC ambayo ni kampuni tanzu ya Atlas Mara, inajivunia ushindi huo ambao ni wa mara ya pili.

"Benki yetu imejishindia tuzo hiyo ya Visa kutokana na matumizi ya kadi zake za Visa ambazo wateja wanatumia kulipia huduma mbalimbali kwa njia ya mtandao," alisema.

Alisema mwaka 2016, BancABC Tanzania ilishinda tuzo hiyo kwa kuongoza kwenye matumizi ya kadi zake za Visa kutumika kwenye kulipia huduma kwa njia ya mtandao.

"Bila nyinyi tusingeweza kushinda tuzo hii na tunawahakikishia wateja wetu kuwa tutaendelea kutoa huduma za kipekee ili kuendelea kuweka imani kwa wateja wetu," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za kidijitali wa benki hiyo, Silas Matoi, alisema wanajisikia fahari kuendelea kuwahudumia wateja na kuwaahidi kuleta huduma bora zaidi.

Naye Meneja Mkazi wa kampuni ya Visa Tanzania, Olive Njoroge, aliwashukuru BancABC Tanzania kwa juhudi kubwa ambazo wamezieweka katika kujitangaza na kuwafahamisha wateja wao kuwa unaweza kutumia kadi ya Visa kwenye kulipia bidhaa au huduma.

# Kenya yashutumu Somalia kuvamia ardhi yake

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta ameinyooshea kidole cha lawama Somalia akisema hatua ya wanajeshi wa Somalia kuingia Kenya ni kitendo cha uchokozi, na kubaini kwamba Kenya haitoendelea kuvumilia hali hiyo.

Jumatano wiki hii, Rais Kenyatta aliitisha kikao cha dharura cha baraza lake la usalama la kitaifa siku mbili baada ya mapigano yaliyotokea Machi 2 kati ya jeshi la Somalia na lile la jimbo Jubaland, mapigano ambayo yalitokea karibu na mpaka na Kenya.

Serikali ya Kenya imeishtumu Mogadishu kwa kukiuka sheria na uhuru wake na kuingia nchini humo.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na maofisa wa Kenya, mapigano kati ya wanajeshi wa Somalia na wale wa Jubaland yalisababisha askari wa Somalia kuingia katika mji wa mpaka wa Kenya wa Mandera, ambapo waliharibu mali za raia na waliwatishia usalama wakazi wa mji huo.

Kenya imesema katika taarifa iliyoitoa kwamba kitendo hicho cha uchokozi hakitoendelea kukifumbia macho.

Wabunge kutoka mji wa Mandera waliliambia Shirika la Habari la AFP siku ya Jumatatu kwamba mashambulizi hayo yalikuwa mabaya hali iliyowafanya wakazi kuyatoroka makazi yao wakihofia usalama wao.

"Acheni uchokozi wa mara kwa mara na badala yake angazieni mambo yenu ya ndani", Kenya haitakubali kutumika kama sababu ya changamoto zinazoikumba Somalia kisiasa," alisema Rais Kenyatta na kuongeza:

"Kenya imelazimika kuathirika pakubwa kutokana na hatua yake ya kuendelea kutoa mchango mkubwa katika kuweka amani na usalama katika nchi jirani ya Somalia" alisema Rais Kenyatta.

Mapigano hayo ya Somalia ni kisa cha hivi karibuni cha wasiwasi kati ya Mogadishu na serikali zake za kijimbo.

Mamlaka ya Jubaland mnamo Agosti, mwaka jana iliishutumu Mogadishu kwa kuingilia uchaguzi wake na kutaka kumpindua madarakani Rais wake, Ahmed Madobe ili kuweza kujipatia uwezo wa kulidhibiti jimbo hilo.

Katika taarifa iliyotolewa Jumanne asubuhi wiki hii, Umoja wa Mataifa (UN) ulisema watu 56,000 walilazimika kuyatoroka makazi yao nchini Somalia kwa sababu ya mvutano katika Jimbo linalojitawala la Jubaland.

**RFI**

# Walioambukizwa corona Afrika wafikia 26, IMF yatoa Sh. bil 50

**WASHINGTON, Marekani**

HADI kufikia jana idadi ya watu walioambulizwa virusi vya ugonjwa wa Corona katika nchi mbalimbali Afrika imefikia 26.

Kati ya idadi hiyo, Algeria ndiyo inaongoza kwa kuwa na idadi wengi ya wagonjwa walioambukizwa ambayo ni 17.

Senegal inashika nafasi ya pili kwa kuwa na wagonjwa wanne waliaombukizwa, wakati Misri ikiwa na wagonjwa wawili, Morocco, Nigeria, Tunisia zikiwa na mgonjwa mmoja.

China ambako ndiko kitovu cha kusambaa kwa virusi hivyo, hadi kufikia jana idadi kubwa ya wananchi walikuwa wameambukizwa licha ya taarifa kuwapo za kupungua kwa maambukizi.

Wakati huohuo, Shirika la Fedha Duniani (IMF) limetangaza kutoa dola za Marekani bilioni 50 kuzisaidia nchi zilizoathirika na virusi vya corona.

Shirika hilo limetoa onyo kuwa mlipuko wa corona tayari umeathiri ukuaji wa kiuchumi wa mwaka huu ukilinganisha na mwaka jana.

Hatua za dharura zimeanza baada ya virusi hivyo kusambaa nje ya China na kuzifikia zaidi ya nchi 70.

Mwanzoni mwa wiki hii, benki ya dunia imechukua hatua ya kupunguza makali ya matokeo ya virusi hivyo.

IMF ilisema kuwa inatoa fedha kwa ajili ya kuwasaidia nchi maskini na kipato cha kati ambazo mifumo ya huduma zao za afya iko chini.

Ilieleza kuwa ufadhili huo utasaidia kukabiliana na janga la kiuchumi kwa sababu kusambaa kwa virusi hivyo kumesababisha uchumi wa dunia kuyumba zaidi mwaka huu wakati janga hilo la kifedha lilianza kushuka taratibu tangu mwaka 2008.

Lakini mkurugenzi wa IMF, Kristalina Georgieva alitoa onyo kuwa si rahisi kujua madhara yatakuwa makubwa kiasi gani na kueleza kuwa ukuaji wa kiuchumi duniani kwa mwaka 2020 utashuka ukilinganisha na mwaka jana.

Hata hivyo, hakuzungumzia kuhusu janga hilo la kiafya kama linaweza kusababisha uchumi wa dunia kushuka.

Jumanne Benki kuu ya Marekani ilipunguza kiwango cha riba ikiwa ni hatua ya kupunguza mzigo wa athari za kiuchumi kutokana na virusi vya corona.

Hiyo ni hatua ya kwanza ya dharura ya kupunguza kiwango cha riba tangu janga la kifedha lianze mwaka 2008.

Siku hiyo hiyo Australia na Malaysia nazo zilipunguza kiasi cha riba kutokana na mlipuko huo.

Mawaziri wa Fedha kutoka mataifa makubwa duniani ya G7 wamehaidi kuweka sera nzuri ambazo zinaweza kukabiliana na athari hizo za kiuchumi zilizotokana na maambukizi ya virusi vya corona.

Mwanzoni mwa wiki, Benki ya Dunia (WB) iliahidi kutoa msaada wa dola bilioni 12 kwa mataifa yanayoendelea kukabiliana na maambukizi ya corona.

Msaada huo wa dharura unajumuisha mikopo ya gharama za chini, ufadhili na msaada wa kiteknolojia. ***BBC***



Wahamiaji na wakimbizi kutoka Syria wanaotafuta hifadhi katika nchi za Ulaya wakivuka mpaka wa eneo la Maghari-bi mwa Uturuki na Ugiriki. **PICHA: REUTERS**

# Uchaguzi Marekani: Bloomberg ajiondoa amuunga mkono Biden

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA aliyekuwa anawania uteuzi wa chama cha Democratic kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa Marekani, Michael Bloomberg, ametangaza kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho baada ya kufanya vibaya katika uchaguzi wa awali uliofanyika Jumanne.

Bloomberg, ambaye hakupata mjumbe yeyote katika uchaguzi wa jana maarufu kama "Super Tuesday," alitangaza kumuunga mkono aliyekuwa Makamu wa Rais, Joe Biden.

Bloomberg aliyeingia katika kinyang'anyiro hicho miezi mitatu iliyopita na kutumia dola nusu bilioni katika kampeni, alisema amejiondoa kwenye kinyang'anyiro ili kuweka mazingira mazuri zaidi ya mgombea wa chama cha Democratic kumshinda Rais Donald Trump katika uchaguzi wa Novemba 2020.

Katika kinyang'anyiro hicho, Bloomberg, hakupata ushindi katika jimbo jingine zaidi ya eneo la American Samoa, lililo kwenye bahari ya Pacific.

Rais Trump ambaye alikuwa akifuatilia matokeo kwa njia ya Televisheni aliandika ujumbe wa kejeli kwa njia ya Twitter akimkosoa mgombea Elizabeth Waren kwa kushindwa kupata ushindi hata katika jimbo lake la nyumbani la Massachusetts.

Biden aliujibu ujumbe huo kwa kuandika: "Njoo Novemba, tunakwenda kukushinda!"

Aliyekuwa Makamu wa Rais, Joe Biden amepata ushindi mkubwa wa majimbo tisa kati ya 14, katika uchaguzi wa Jumanne, akifuatiwa na seneta Bernie Sanders.

***DW***

# TCRA kushindanisha watoa huduma za mawasiliano

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewahimiza watoa huduma za mawasiliano wenye leseni za mamlaka hiyo kushiriki tuzo za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama).

Akizungumza kwenye mkutano wa waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, James Kilaba alisema wanaelekea mwisho mwa uwasilishaji wa nia ya kushiriki tuzo hizo ambayo itakuwa Machi 15.

Alisema tukio hilo ni la kwanza kuandaliwa hapa nchini na nia ni kuwatambua na kuwatunuku watoaji huduma bora za mawasiliano ili waongeze ubunifu katika utoaji wa huduma za utangazaji.

Kilaba alisema nia ya tuzo hizo ni kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za mawasiliano katika sekta za posta, simu, utangazaji na intaneti na kuongeza chachu na mchango wa sekta ya mawasiliano.

"Kwa mfano wenye leseni za TCRA wote wanatakiwa kuomba kushiriki katika tuzo hizi kwa muda uliowekwa na wananchi watahimizwa kupiga kura ya mtoa huduma anayetoa huduma nzuri zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Tehama (TCRA), Connie Francis, alisema kutakuwa na tuzo 17 kwenye shindano hilo wakiwamo watoa huduma bora wa simu, watoa huduma bora wa intaneti na mtoa huduma bora wa miundombinu ya utangazaji.

Alisema wengine ni mtoa maudhui mtandao bora wa blog, kituo bora cha utangazaji wa televisheni kitaifa, kituo bora cha utangazaji wa televisheni kiwilaya, chaneli bora ya kitaifa inayotazamwa kwa kulipia na mtoa maudhui mtandao bora wa televisheni.

Connie alisema mchujo wa awali kwenye tuzo hizo utafanyika mwezi huu ambapo idadi ya mawasilisho yaliyochaguliwa yatachapishwa kwenye tovuti ya mamlaka hiyo.

Alisema kuanzia mwezi Aprili wananchi watapiga kura kwa njia ya mtandao kwa kupitia tovuti ya TCRA na kwa kutuma ujumbe mfupi kwenye namba ya bure waliyoiweka.

Aliongeza kuwa uteuzi wa mwisho utajumuisha mapendekezo ya kura za wananchi pamoja na usaili utakaofanywa na jopo la majaji hatua ambayo itafanyika kuanzia Mei 2 hadi Mei 10, mwaka huu.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Amos Nungu (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya Wiki ya Ubunifu na Ikolojia, inayoanza Machi 8 mwaka huu. Kulia ni Naibu Kiongozi wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uingereza (DFID), Natalie Smith na Mkurugenzi wa Uhusiano wa Vodacom, Rosalynn Mworia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wauza rangi wajivunia mchango wao kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya rangi ya Coral Paints imesema miaka 30 ya uwapo wake nchini umeiwezesha kushiriki katika kukuza uchumi wa Watanzania na taifa kwa ujumla.

Pia imejivunia mchango wake katika kuwainua wajasiriamali kwa ajira katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya maadhimisho hayo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Kishan Dhebar, alisema wengi miongoni mwa wajasiriamali hao kwa sasa ni mawakala wakubwa wa ndani na nje ya nchi.

"Wapo ambao tulianza nao miaka 30 iliyopita na tumekuwa tukitumia takribani Sh. milioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kuwainua wajasiriamali wa Tanzania. Hadi sasa tuna takriban mawakala 1,500 ndani na nje ya nchi," alisema Dhebar.

Dhebar alisema Coral Paints katika miji ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Moshi ambako ndiko kampuni hiyo ilikozaliwa mwaka 1990, ikiasisiwa na Watanzania kabla ya kupanuka na kuwa kinara katika soko la rangi, ikichagizwa na kauli mbiu ya 'Kupamba na Kusherehekea'.

Akizungumzia mafanikio ya kampuni kwa miaka yake 30, mmoja wa wafanyakazi, Amani Mosha, alisema iikuwa ni miaka ya kujivunia kutokana na ubora wa bidhaa wanazozalisha na kuziingiza sokoni.

Misha alisema zao ni bora na kukidhi matakwa ya wateja ikionyesha thamani halisi ya nyumba au gari.

# Wabunifu 6,000 kushiriki Wiki ya Ubunifu

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya wabunifu 6,000 wanatarajia kushiriki katika wiki ya ubunifu mwaka huu inayotarajiwa kuanza Machi 8 hadi 13, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Wiki ya ubunifu inatarajia kuambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo maonyesho ya kazi za kibunifu kutoka kwa wadau mbalimbali wa ubunifu nchi nzima.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia(COSTECH), Dk. Amos Nungu, alisema wiki ya ubunifu nchini imefanyika kwa miaka sita mfululizo na inaandaliwa na Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Binadamu (HDIF) na Ukaid, kwa kushirikiana na tume hiyo na kufadhiliwa na wadau wengine wa maendeleo wakiwamo, UNDP, Unicef, UN Women, UNCDF, na Vodacom Tanzania.

Dk. Amos Nungu alisema mbali na maonyesho hayo, lakini wabunifu watapata fursa ya kubadilishana mawazo na kujifunza kazi mbalimbali za kibunifu.

"Wiki ya ubunifu mwaka huu inabeba kaulimbiu inayosema 'buni kwa tija' lengo ni kukuza na kuendeleza bunifu kwa maendeleo ya watu na kuhakikisha tunavitambua na kuendeleza vipaji na kazi zote za kibunifu," alisema Dk. Nungu.

Aliema mwaka jana wiki ya ubunifu ilifanyika katika mikoa mitatu pekee, na kwamba mwaka huu wameiboresha zaidi na itafanyika katika mikoa sita ikiwamo Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya na Iringa.

Alisema tangu kuanza kufanyika kwa wiki za ubunifu, kumesaidia kuleta mafanikio katika sekta ya ubunifu.

"Serikali tunathamini sana ubunifu na ndiyo maana tumeendelea kuendesha wiki hizi kwa miaka sita mfululizo, kuna hatua kubwa tumefikia, kwa sasa tunashuhudia vitu vingi vinavyotokana na ubunifu na tunajivunia hilo na ndiyo maana tunasisitiza watu wabuni kwa tija," alisema Dk. Nungu.

Mkurugenzi Mkazi wa HDIF, Joseph Manirakiza, alisema wanafurahi kuona wiki hiyo ambayo imekuwa ikifanyika kila mwaka kuendelea kuwa na mafanikio makubwa na kuongezeka kwa ushiriki wa watu kila.

Kaimu Kiongozi wa Jopo kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo (DFID), Natalie Smith, alisema ili taifa lolote liendelee, linahitaji ubunifu.

Mwakilishi wa UNDP, Sergio Valdini, alisema wanadhamini kwa mara ya kwanza baada ya kuona umuhimu wa bunifu katika maendeleo ya nchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

## KUPOTEA KWA CHETI



MOHSIN MSUYA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1071-0374** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2004 katika shule ya Sekondari St. Matthew.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/CHA/RB/160286/2019

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;63/2020

Ombi la BAHATI MAMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/03/2020.

115657702

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;66/2020

Ombi la PILI WAZIRI MKANGU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu WAZIRI MJANGU SUME.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/03/2020.

115657802

---

## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

Taasisi ya Serve and Save Children Tanzania inatangaza kupotea kwa cheti cha Usajili chenye namba ya Usajili **00NGO/00010154** kilichotolewa na wizara ya Maendeleo ya Jamii.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi au Wasiliana na namba ya simu 0655 899860

156572

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
04/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 07/03/2020 kampuni ya **CIVIL LOTHS ENTERPRISES LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **SONGEA** kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lina namba za usajili: **T392 DPZ/ T 295 DGR**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **17.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: SONGEA hadi **DAR ES SALAAM** kupitia LINDI *Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115656802

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**TAXATION CAUSE No. 3 OF 2019**

**HAJINAS ONESPHORY ........................DECREE HOLDER**

**VERSUS**

**TANZANIA DAIMA NEWS PAPER ...........1st JUDGEMENT DEBTOR**
**ABSALOM KIBANDA ................2nd JUDGEMENT DEBTOR**
**MBEKI MBEKI ............................3rd JUDGEMENT DEBTOR**
**ANTIDIUS KALUNDE ................4th JUDGEMENT DEBTOR**
**FREE MEDIA LIMITED ..............5th JUDGEMENT DEBTOR**

Notece To Show cause why Bill of Costs should not be Granted to **TANZANIA DAIMA NEWS PAPER, ABSALOM KIBANDA, FREE MEDIA LIMITED.**

Whereas *plaintiff (Decree Holder) has made application to this Court for Bill of Costs in the Civil Case No.35 of 2017. This is to give you notice that you are to appear before this Court on the 18th day of March, 2020 to show cause why Bill of Costs should not be granted.

**GIVEN** under my hand and the SEAL of the Court, this **3rd day of March 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE BUKOBA
TAXING MASTER

215656702

---

Uza, Chenye Thamani

Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi

Kwa

Bei Poa Tupigie

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# DE BRUYNE HATIHATI KUIVAA UNITED

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola hana uhakika kama Kevin De Bruyne atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa 'dabi' ya keshokutwa Jumapili dhidi ya Manchester United kutokana na kuumia bega.

De Bruyne hakuwapo katika kikosi cha City kilichoibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sheffield Wednesday kwenye mchezo wa Kombe la FA juzi, huku bao la Sergio Aguero likiwapeleka kwenye robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza baada ya ushindi huo wa Jumatano, Guardiola alibainisha kwamba, De Bruyne alikosekana kwa sababu ya maumivu aliyoyapata kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Aston Villa wikendi iliyopita.

Bosi huyo wa City alibainisha hajui kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atakuwa tayari kwa ajili ya mchezo huo wa miamba ya jiji moja la Manchester utakaopigwa katika kwenye Uwanja wa Old Trafford.

"Kevin alikuwa na tatizo kwenye bega," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari. "Hakuwa fiti.

"Katika mchezo uliopita, dakika ya mwisho alianguka chini vibaya na alikuwa na matatizo ya mgongo. Hatujui atakuwa nje kwa muda gani. Matumaini yetu sio kwa muda mrefu."

Alipoulizwa kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji atakuwa fiti kwa ajili ya mchezo dhidi ya United, alijibu: "Sijui."

## DIER AMRUKIA SHABIKI JUKWAANI

**LONDON, England**

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Eric Dier aliruka uzio na kwenda jukwaani kutaka kuzichapa na shabiki wakati wa mchezo wa Kombe la FA, uliochezwa juzi Jumatano.

Tukio hilo lilitokea wakati Tottenham ikitolewa nje kwa kufungwa mabao 3-2 katika changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya kutoka sare ya 1-1 dhidi ya Norwich City.

Dier alikwenda kwa kasi jukwaani kumvaa shabiki huyo kabla ya maofisa usalama kumzuia.

"Nadhani Eric amefanya jambo ambalo kwa mchezaji wa kimataifa hawezi kutenda, lakini kila mmoja anaweza kufanya," alisema kocha Jose Mourinho.

Dier aliyecheza mechi 40 za England alishindwa kuisaidia Spurs kusonga mbele katika mashindano hayo baada ya kipa wa Norwich Tim Krul kuokoa penalti mbili.

Norwich inashika mkia katika msimamo wa Ligi Kuu England na matokeo hayo yamewachukiza mashabiki wa Spurs.

"Narudia kusema mchezaji wa kimataifa hapaswi kufanya vile, lakini narudi jambo hili linaweza kufanywa na yeyote," alisisitiza Mourinho.

Alisema lugha ya maudhi iliyotolewa na shabiki huyo ilikuwa ya kumchukiza mchezaji huyo kwa kuwa familia yake ilikuwa uwanjani.

Katika mechi nyingine, Leicester City iliichapa Birmingham bao 1-0 na kusonga mbele.

## Barca kumtumia Vidal chambo kumnasa Martinez

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imejipanga kweli kweli kuimarisha safu yake ya ushambuliaji katika usajili wa majira ya joto yajayo kwa kuongeza kasi ya kuwania kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Barcelona katika harakati hizo imetoa ofa ya euro milioni 70 pamoja na kuwatoa chambo wachezaji wawili wa timu hiyo ambao kiungo Arturo Vidal pamoja na beki wa kulia, Nelson Semedo.

Mkataba wa Martinez unakipengele kinachosema kuwa timu yoyote inayomtaka inatakiwa kukamilisha usajili wake kati ya Julai 1 hadi Julai 15 mwaka huu kwa dau la euro milioni 111.

Dau hilo ni kubwa Barcelona na ndiyo maana imeamua kuwajumuisha Vidal na Semedo katika ofa yake, ikiamini kuwa uwepo wao utaishawishi Inter kulegeza masharti na kupokea hizo euro milioni 70.

Jumapili Barcelona ilipata kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Real Madrid na sasa wameona mapungufu yao.



HABARI MICHEZO



# SOLSKJAER AMTABIRIA MAKUBWA ROONEY

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anaamini mfungaji wa wakati wote na nahodha wa zamani, Wayne Rooney anaweza kuwa kocha wa timu hiyo katika siku za usoni.

Rooney jana Alhamisi alikutana na United wakati timu yake ya Derby County ilipokikaribisha kikosi hicho cha Solskjaer pale kwenye Uwanja wa Pride Park katika raundi ya nne ya Kombe la FA.

Mshindi huyo mara tano wa Kombe la Ligi Kuu na mara moja Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya kuondoka United mwaka 2017, Rooney alijiunga na Derby kabla kocha mchezaji akitoka kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, katika klabu ya DC United Januari.

"Ndio," Solskjaer alijibu wakati alipoulizwa kama Rooney mwenye umri wa miaka 34 anaweza kuwa kocha.

"Inategemea kwa namna gani anajiwekeza kwenye kazi na vipi unaipenda kazi hiyo.

"Inachukua maisha yako, lakini ni kazi ya pili nzuri baada ya kucheza soka kwa muda mrefu. Nina uhakika wachezaji wengi wa zamani na makocha wanaoitaka kazi yangu."

Rooney ndiye mchezaji anayeongoza kwa kuifungia mbao mengi United akiwa ametikisa nyavu mara 253 katika mechi 559 alizowachezea miamba hao wa Ligi Kuu England.

***

# Tuchel asifia 'pacha' ya Neymar, Mbappe

**PARIS, Ufaransa**

THOMAS Tuchel amemsifia shujaa wa 'hat-trick', Kylian Mbappe kwa kurudi kwenye kiwango chake baada ya kuwa kwenye wakati "mgumu" dhidi ya Borussia Dortmund, huku upatina wake na Neymar ukisaidia zaidi Paris Saint-Germain.

Wakati PSG wakitumia mfumo wa 4-3-3, Mbappe alishindwa kufanya lolote kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 kule Dortmund mwezi uliopita.

Hata hivyo, tangu kichapo cha 2-1 kwenye michuano hiyo ya Ulaya, mshambuliaji huyo wa Ufaransa Mbappe, amefunga mabao sita katika mechi tatu za nyumbani.

Mbappe alifunga hat-trick Jumatano kuisaidia PSG kutinga fainali ya Kombe la Coupe de France, huku Tuchel akimsifia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kwa kiwango alichoonyesha wakati wakiibuka na ushindi wa 5-1 dhidi ya Lyon.

"Mbappe amekuwa imara sana kwa wiki chache zilizopita. Alikuwa na wakati mgumu wakati tukicheza kule Dortmund, akicheza katika nafasi tofauti. Kwa uhakika ilikuwa ngumu dhidi ya Dortmund," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa uwepo wa Neymar, wako imara sana pamoja. Baada ya Dortmund, Mbappe alionyesha uwezo wake kwenye mechi dhidi ya Dijon na Lyon.

"Yupo imara, anatumia kasi yake vizuri sana, ana maamuzi ya haraka. Kwa uhakika kabisa yupo vizuri."



# Inter yachangia Euro 100,000 utafiti wa corona

**MILAN, Italia**

INTER Milan na Rais Steven Zhang wametoa mchango wa Euro 100,000 kwa ajili ya kufanyika kwa utafiti wa ugonjwa wa corona, klabu hiyo ya Ligi Kuu England, Serie A, imetangaza.

Nerazzurri wametoa mchango huyo kwa Idara ya dawa na sayansi kwenye hospitali ya Sacco iliyopo mjini Milan ili kusaidia kumaliza mlipuko wa ugonjwa huo.

Ugonjwa wa corona umesababisha mechi za Serie A na matukio yote ya kimichezo nchini Italia kufanyika bila mashabiki kwa milango yake kufungwa hadi Aprili 3 mwaka huu kwa amri ya serikali.

Mechi za Serie A zilifutwa kwa wikendi mbili zilizopita, pamoja na mchezo wa nusu fainali wa Kombe la Coppa Italia uliotakiwa kuchezwa Jumatano.

"Inter imeamua kutoa ushirikiano wake kwa jiji la Milan na inajivunia kutoa mchango wake kwenye kitengo cha utafiti wa magonjwa katika hospitali ya Sacco," alisema Rais Steven Zhang.

"Tangu mlipuko wa ugonjwa wa corona, tulifuata maagizo ya serikali na tunatoa ushirikiano kwa asilimia zote.

Hadi sasa zaidi ya watu 2,502 wamethibitika kuwa na virusi vya ugonjwa huo nchini Italia, huku vifo 80 vikiripotiwa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DORTMUND YAJIPANGA KUMSAJILI BELLINGHAM

●●●Ni kiungo aliyeonyesha kiwango kizuri akiwa na City na anayewaniwa na klabu mbalimbali za…

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund inaamini itafanikiwa kupata saini ya kiungo chipukizi wa Birmingham City, Jude Bellingham katika kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo bado Borussia Dortmund haijaafikiana chochote na Birmingham City kuhusu uhamisho wa chipukizi huyo mwenye umri wa miaka 16 ambaye anaichezea timu hiyo inayoshiriki Ligi ya Championship.

Katika umri wake huo, Bellingham amekuwa mmoja wa wachezaji walioonyesha kiwango cha juu katika soka la Uingereza, ingawa kinda huyo hawezi kusaini mkataba wa kuanza kucheza soka la kulipwa mpaka atakapofikisha miaka 17, hapo Juni 29, mwaka huu.

Birmingham inajiandaa kupata dau la pauni milioni 35 katika mauzo ya mchezaji huyo.

Kiwango cha Bellingham pia kimezifutia klabu mbalimbali za England na Ulaya zikiwamo Manchester United, Chelsea, Liverpool, Bayern Munich na Juventus.

Dortmund inajulikana kuwa ni moja ya sehemu sahihi inayosifika duniani katika kuendeleza vipaji vya wachezaji chipuziki. Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho na straika wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Haaland ni wachezaji wawili wanaotamba ambao waliwindwa na timu mbalimbali lakini walichagua kutua katika klabu hiyo ya Bundesliga na kuzikacha nyingine.

Katika kikosi cha Birmingham, nyota huyo alipata mafanikio zaidi akichezeshwa katika nafasi ya kiungo, lakini Dortmund inajipanga kumtumia kwenye nafasi ya kiungo mshambuliaji wa kati.

Mchezaji mwenyewe pia anaonekana anavutiwa na maendeleo ambayo ameyapata Sancho ndani ya kikosi cha Dortmund.

Wakati Sancho anaondoka Manchester City na kujiunga na klabu hiyo ya Ujerumani mwaka 2017, alikuwa tayari ameshakuwa mchezaji mwenye kiwango kizuri, lakini ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita, kwa sasa mshambuliaji huyo ameimarika zaidi na amekuwa mmoja wa wachezaji nyota barani Ulaya.

Bellingham hakuwa sehemu ya kikosi kilichoshuka dimbani katika mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA iliyochezwa Jumatano iliyopita dhidi ya Leicester, baada ya Kocha wa City, Pep Guardiola kuamua kutomjumuisha ili apate nafasi ya kupumzika kutokana na kumchezesha mechi 34 msimu huu.

Pep alisema, "Ninataka mchezaji wangu apate muda wa kutosha wa kupumzika, ili Jumamosi awe na nguvu mpya. Najua hili halitawafurahisha mashabiki wetu, lakini ukweli ni kuwa hawezi kucheza dhidi ya timu pinzani ya Ligi Kuu England. Ni rahisi sana, wachezaji wenzake wanajua wanahitaji kupata ushindi, kwa hiyo nitachezesha kikosi kingine kwa ajili ya kusaka ushindi kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu."

## KWA UFUPI

**KANE ANUKIA UNITED**

STRAIKA wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane (26), anatarajia kukubali ofa ya kwenda kujiunga na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. Nyota huyo ametajwa hana mpango wa kusaini mkataba mpya na Spurs. ***(Goal)***

**ARSENAL KUMKARIBISHA STONES**

ARSENAL inatarajia kumpa ofa beki wa Timu ya Taifa ya England, John Stones ambaye ana umri wa miaka 25, ili kuzuia mchakato wa kuelekea Manchester City mwishoni mwa msimu huu. ***(90 Min)***

**WERNER MAMBO BADO**

MKURUGENZI wa Michezo wa RB Leipzig amesema klabu hiyo haijapokea ofa yoyote rasmi ya kumhitaji straika wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner (23), licha ya kutajwa kutakiwa na Liverpool, Chelsea na Manchester United. ***(Mirror)***

**ANGELINO AITEGA CITY**

BEKI wa kushoto wa Manchester City Mhispania Angelino (23), ambaye yuko kwa mkopo RB Leipzig, amesema ataondoka City kama kifungo cha kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kitaendelea kuikabili timu hiyo. ***(MEN)***

**UNITED YAINGIA SOKONI**

MANCHESTER United imetajwa pia inampango wa kuwania saini ya Jude Bellingham. Lakini taarifa kutoka katika klabu yake ya Birmingham zinasema hakuna ofa yoyote iliyotua kumwitaji kinda huyo. ***(MEN)***

**DORTMUND YAMTAKA SANCHO**

KLABU ya Borussia Dortmund imeweka dau la pauni milioni 121 ili kuwania saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Bild - in German)***

**WILLIAN KUTUA SPURS**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea Mbrazil Willian (31), anajiandaa kukaa kusaini mkataba mpya na klabu yake hiyo na anatajwa kuwa na mpango wa kujiunga na Tottenham katika majira ya joto. ***(UOL)***

**TELLES KUMRITHI ALONSO**

CHELSEA inatakiwa kulipa zaidi ya pauni milioni 40 ili kupata saini ya beki wa Porto na Timu ya Taifa ya Brazil, Alex Telles (27), kama mrithi wa beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania Marcos Alonso, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Sun)***

**RAKITIC AKARIBIA ATLETICO**

ATLETICO Madrid inatajwa kuwa na mpango wa kumsajili kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (31), katika majira ya joto. ***(Marca - in Spanish)***

**WANYAMA KUHAMIA MONTREAL**

TOTTENHAM imemkubalia kiungo wa Timu ya Taifa ya Kenya, Victor Wanyama (28), kujiunga na Montreal Impact kwa usajili huru licha ya klabu hiyo kuhitaji kulipwa ada ya pauni milioni 9 katika dirisha dogo la Januari. ***(Standard)***

**MILAN YAIBANA BARCA**

INTER Milan itahitaji wachezaji watatu kutoka Barcelona kama mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania wataendelea na nia ya kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez (22), katika majira ya joto. ***(Mundo Deportivo, via Mail)***

**ARTETA AMTAKA CAMARA**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anataka klabu hiyo imsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Guinea na Olympiacos, Mady Camara, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Sdna, via Star)***

HABARI MICHEZO

# DILUNGA AFUNGUKA SIMBA YATAKA UBINGWA MAPEMA

**Na Saada Akida**

NJIA nyeupe! Kiungo wa Simba, Hassan Dilunga amesema baada ya kuwafunga Azam FC, sasa wanahitaji pointi nyingine tatu muhimu kutoka kwa Yanga ili kujihakikishia nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu mapema.

Ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam, ambao Simba iliupata katika mchezo wa juzi uliopigwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, umewafanya vinara hao kufikisha alama 68 katika michezo 26 ya ligi hiyo waliyocheza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dilunga alisema malengo yao makubwa yalikuwa ni kuhakikisha washinda mechi dhidi ya Azam na Yanga na kuukaribia ubingwa kabla ya wachezaji hawajaelekea katika kambi ya timu ya Taifa (Taifa Stars), kwa ajili ya kuelekea kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Dilunga alisema walipambana kukabiliana na ushindani uliokuwapo katika mchezo huo na wamepanga kuendelea kucheza katika kiwango bora na hatimaye kupata pointi nyingine tatu dhidi ya Yanga.

"Malengo yetu ni kushinda mechi mbili hizi ambazo nina uhakika pointi tutakazozipata zitatuweka katika mazingira mazuri ya kutangaza ubingwa mapema," alisema Dilunga.

Kiungo huyo alisema pia mipango ya kutafuta pointi hizo sita kutoka kwa Azam na Yanga iliandaliwa mapema kwa sababu wanataka kuona wakirejea kutoka kwenye fainali za CHAN, wataikuta vita hiyo ya kuwania ubingwa imekolea.

Ligi Kuu Bara itasimama kwa muda ili kupisha kikosi cha Taifa Stars kwenda Cameroon kupeperusha bendera ya nchi katika fainali hizo za CHAN zitakazofanyika kuanzia Aprili 4 hadi 25 mwaka huu na Tanzania iko katika Kundi D pamoja na Guinea, Zambia na Namibia.



Wachezaji wa Simba wakishangilia bao la ushindi lililofungwa na Meddie Kagere ( wa pili kutoka kulia) katika mchezo wa Ligi Kuu uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. Wengine kutoka kushoto ni John Bocco, Luis Miquissone na Shomary Kapombe. Simba ilishinda mabao 3-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kelvin atamba kuibakisha Mbeya City

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MSHAMBULIAJI chipukizi wa Mbeya City, Kelvin John, ametamba ataendelea kuisaidia timu yake kwa kufunga mabao muhimu na hatimaye kusalia katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kelvin alisema hayo baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 3-2 dhidi ya Kagera Sugar hapo juzi.

"Namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kufunga mabao mawili na kuiwezesha timu yangu kupata pointi tatu muhimu, nimefurahi kurudi nyumbani Kaitaba na kufanikiwa kuutumia vizuri uwanja huu ambao nimeuzoea kiasi," alisema Kelvin.

Alisema nia yake ni kuendelea kupambana ili afunge mabao mengi katika mechi zilizosalia, kwa lengo la kujiweka katika nafasi nzuri ya ufungaji katika Ligi Kuu Tanzania Bara, na kuinusuru timu yake isishuke daraja.

"Hatuna hofu ya kushuka daraja maana mechi zote tumecheza vizuri na yanayotokea ni matokeo tu, tutajitahidi kucheza vizuri mechi zilizobaki ili tupate ushindi na kubakiza timu yetu katika Ligi Kuu msimu ujao," Kelvin alisema.

Kocha Msaidizi wa Mbeya City, Mohamed Kijuso alikiri ligi ni ngumu na kikosi chake kinatakiwa kujizatiti zaidi kutokana na kuwa katika nafasi mbaya kwenye msimamo wa ligi.

"Tumekuja Kagera tukiwa na pointi 24 na sasa tunaondoka tukiwa na pointi 27, ulikuwa mchezo mgumu, lakini vijana wangu wamepambana kusaka ushindi kwa kutambua tuko katika nafasi mbaya, tunafurahia ushindi maana Kagera ni timu nzuri na kuifunga katika uwanja wake wa nyumbani sio mchezo," alisema Kijuso.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema mechi haikuwa ngumu sana kwao na kuwa walipoteza pointi tatu nyumbani kutokana na kukosa umakini.

"Mechi iliyopita tulifungwa mapema na suala hili tukalifanyia kazi, lakini nashangaa limejirudia tena tukafungwa bao la kwanza mapema zaidi, tunaendelea kulifanyia kazi tatizo hili, ili kuiweka timu sawa," alisema Mexime.

Alisema safu yake ya ulinzi haikuwa imara lakini anaahidi kuifanyia kazi ili kutorudia makosa yake katika mechi inayofuata.

## Jang'ombe Boys yalalamikia ratiba

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Jang'ombe Boys inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar imesema ratiba ya ligi hiyo si 'rafiki' na hali hiyo inapelekea wachezaji wao kucheza kwa kiwango cha chini.

Katibu Mkuu wa Jang'ombe Boys, Abdallah Mahfoudh "Dallas" alisema ratiba ya mechi za ligi hiyo imebanana na inapelekea wachezaji wake kukabiliwa na uchovu na kushindwa kufanya vema katika michezo inayowakabili.

"Tunacheza mechi nyingi na zinachezwa mfululizo, hali hii inapelekea timu kutofanya vizuri na hata kuwa na majeruhi wengi, inatuumiza na itatufanya tunapoteza mechi au kuambulia sare," alisema Dallas.

Aliongeza mwenendo wa ratiba ya ligi hiyo haitoi nafasi kwa timu kujiandaa na michezo inayofuata na hivyo wachezaji wanashinda kuonyesha uwezo wao halisi.

"Ratiba imebana sana, kila baada ya siku moja timu inatakiwa iingie uwanjani kucheza, na utakuta kuna mechi ngumu inakukabili mbele yako, pia utakuta ratiba inaonyesha ucheze kiwanja cha Gombani, Pemba na usafiri wetu wa meli ambao unamashaka baharini, hii sio kitu kizuri, " Dallas alisema.

Aliongeza kuwa moja ya sababu za kuwapo ratiba hiyo ni kukosekana kwa wadhamini, hivyo timu zinatakiwa kumaliza ligi mapema ili kuepuka gharama za juu za

## LaLiga yaandaa kongamano Dar

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na LaLiga ya Hispania wameandaa kongamano la michezo ambalo litawashirikisha viongozi wa shirikisho hilo na klabu za Ligi Kuu Bara, imeelezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Masoko wa TFF, Boniface Wambura alisema katika kongamano hilo la siku tatu, washiriki watapata elimu ya utendaji wa shughuli za maendeleo ya soka.

Wambura alisema kongamano hilo litaongozwa na mwakilishi kutoka LaLiga na wanaamini litasaidia kuboresha mbinu za kiutawala na hatimaye kusaidia mpira wa hapa nchini.

"Kongamano hilo litasaidia kukuza soka letu, hasa katika masuala ya utendaji kwa kuendesha soka la kisasa, lakini kwa upande wa shirikisho tutoke huku katika Bodi ya Ligi tufike katika hatua nyingine," alisema Wambura.

Naye Mwakilishi kutoka LaLiga, Alvaro Paya alisema kongamano hilo litagusa mambo mbalimbali ikiwamo utendaji, masoko na namna ya klabu za hapa nchini kujikwamua na kujiendesha kisasa.

# Michezo

Ijumaa Machi 6, 2020

Nipashe




Dortmund yajipanga kumsajili Bellingham

HABARI UK 30

HUPITI



Nahodha wa Azam FC, Aggrey Morris (kushoto), akimiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa Simba, Deo Kanda katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 3-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba yatamba hawatapoa ng'o

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amewapongeza wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango kizuri katika mechi hiyo iliyomalizika kwa kupata ushindi wa mabao 3-2.

Sven alisema licha ya kuchelewa kufika uwanjani na kukosa muda wa kutosha kwa 'kupasha mwili', anashukuru hakuna kilichoharibika na malengo yao ya kupata pointi tatu muhimu yalitimia.

"Nimefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wangu, wametumia maelekezo vizuri na kuweza kuipatia ushindi timu yetu kutokana na nguvu kubwa waliyoifanya, sasa tunajipanga kwa ajili ya mchezo wetu wa Jumapili, siku tatu zinanitosha kukiandaa kikosi changu," Sven alisema.

Mbelgiji huyo aliongeza kikosi chake hakitatoka nje ya Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kuikabili Yanga na anaamini siku tatu zilizoko, zinatosha kujiweka tayari na mchezo huo.

"Kikubwa ni maandalizi ya mchezo husika, lakini kuwajenga kisaikolojia wachezaji wangu, ni mechi ngumu na muhimu ambayo wanahitajika kupambana kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Alifurahi kuona mshambuliaji kinara katika ligi hiyo, Meddie Kagere amefunga bao kwenye mchezo huo wa juzi na hali hiyo imemrudisha katika makali yake ya kufumania nyavu.

# YANGA YACHOCHEA USHINDI JUMAPILI

●●● Yatangaza motisha Sh. milioni 200 endapo itaibuka na ushindi keshokutwa, waamuzi sita wapangwa kuchezesha dabi hiyo...

**Na Somoe Ng'itu**

KATIKA kuhakikisha timu inapata ushindi na kuongeza morali kwa wachezaji wake kuelekea mechi dhidi ya watani zao Simba ambayo itachezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, uongozi wa Yanga umetangaza kutoa motisha ya Sh. milioni 200 endapo watapata pointi tatu muhimu.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema wadhamini wa timu hiyo, GSM imefikia uamuzi huo ili kuhakikisha malengo yao ya kushinda mechi hiyo yanatimia.

Nugaz alisema mbali na kiwango kizuri cha timu yao, wanaamini motisha hiyo ya fedha itaongeza chachu ya kusaka matokeo mazuri na wanawataka mashabiki na wanachama wa Yanga kutohofia mechi hiyo.

Aliongeza kuwa kiwango cha Yanga kimeimarika tofauti na ilivyokuwa miezi mitatu iliyopita hivyo wanaamini wataondoka na furaha na kuendelea kujiimarisha katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo na kumfurahisha mgeni rasmi kutoka CAF.

"Tunapenda kuwaalika mashabiki wa Yanga kuja kwa wingi uwanjani, vaeni jezi zenu mpendeze, bila makandokando, Jumapili tunauhakika tunakwenda kuifunga Simba, bila makandokando, Yanga haifungwi," Nugaz alisema.

Alisema timu yao pia imekuwa ikitoa motisha ya Sh. 100,000 kwa wachezaji kila wanaposhinda katika mechi ya ligi na Sh. 50,000 watapotoka sare na kutoambulia chochote pale timu yao inapopoteza mchezo.

Mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Edibily Lunyamila alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa nzuri kutokana na ushindani wa timu hizo mbili kila zinapokutana.

"Simba wako vizuri kuliko Yanga, wako kileleni, Yanga inajengwa, na itaamuliwa na upande wa viungo, itakuwa na ushindani mkubwa sana," alisema Lunyamila ambaye aliwahi kuzichezea timu zote mbili.

**WAAMUZI SITA KUCHEZESHA**

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema kuwa mwamuzi wa kati katika mechi hiyo atakuwa Martin Saanya kutoka Morogoro ambaye atasaidiwa na Mohammed Mkono na Frank Komba huku Elly Sasii akiwa ni mwamuzi wa akiba.

Abdallah Mwinyimkuu na Ramadhani Kayoko watakuwa katika eneo la magoli na uamuzi huo umewekwa ili kuongeza ufanisi katika mechi hiyo ya marudiano msimu huu.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Januari 4, mwaka huu, refa Jonesia Rukyaa kutoka Bukoba ndiye aliyesimama kati na mchezo huo ulimalizika kwa sare ya mabao 2-2.

**ULINZI KUTAWALA**

Mkurugenzi wa Michezo nchini, Yusuf Singo, alisema serikali imeandaa kuweka ulinzi wa kiwango cha juu katika mechi hiyo kutokana na ugeni wa Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad ambaye anatarajiwa kuhudhuria pambano hilo.

Singo alisema tiketi za eneo la VVIP hazitauzwa na badala yake watakaa wageni maalumu ambao watakuwa wamealikwa ili kuimarisha utulivu.

"Kutakuwa na ulinzi mkali sana pia mabadiliko makubwa katika sehemu ya VVIP, kutokana na ujio wa rais huyo na Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi wa CAF, sehemu ambayo itakuwa ya hadhi ya juu," alisema Singo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohammed Dewji 'Mo' amesema wadau wa soka nchini watamkaribisha na kumpa heshima ya juu Ahmad na wanaamini ujio wake utasaidia kuchochea maendeleo ya soka nchini.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042